epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Desemba 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581885
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

MIEZI MINNE

# Samia ahamisha tena mawaziri



• **Sekta** ya Habari yarudishwa ilikokuwa enzi za JK; Msigwa arejeshewa jukumu la usemaji; Kabudi, Ndumbaro, Bashungwa, Silaa waguswa... *Ukurasa 2*


Dk. Damas Ndumbaro


Dk. Ashatu Kijaji


Abdallah Ulega

> "Rais imempendeza kuirejesha kule pa awali, tunaamini waliopewa dhamana hawataiweka kando Sekta ya Habari kama ilivyokuwa awali. Faraja tuliyoipata ni kwamba viongozi wakuu wote walioteuliwa ni wanahabari.
>
> **Deodatus Balile**


Hamad Masauni


Innocent Bashungwa


Prof. Palamagamba Kabudi


Jerry Silaa

UKURASA WA 2

**ACT** yaamua kwenda kortini kupinga matokeo Uchaguzi S/Mitaa

UONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo umesema hauko tayari kutambua matokeo yote ya Uchaguzi wa Serikali za...

UKURASA WA 18

**Mama** anusurika kuuawa kwa panga na mwanawe

MKAZI wa Kitongoji cha Gudugudu, Kata ya Mlali wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro, Unnu Martin (70), amelazwa...

UKURASA WA 17&19

MIAKA 63 YA UHURU


**Mkuu** Mkoa asimulia mapinduzi yalikofika, ya zamani yamebaki historia kila sekta

LEO inaposherehekewa miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania, kuna mengi mazuri yamesimuliwa...

MAUAJI OFISA TRA

**Waziri Mwigulu aungana na wanaochukua hatua kisheria**

UKURASA 3


UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF INDUSTRY AND TRADE
FAIR COMPETITION COMMISSION
FCC

NOTIFICATION REGARDING THE INTENTION OF UDONGO WETU LIMITED TO ACQUIRE PROPERTIES FROM BOMBAY BURMAH TRADING COMPANY LIMITED

PUBLIC NOTICE

(Made under Section 65 (2) (g) of the Fair Competition Act No. 8 of 2003 and Rules 41 (6), 42 (5) and 49 of the Fair Competition Rules, 2018)

The Fair Competition Commission (FCC) is an independent statutory body established under section 62 of the Fair Competition Act No. 8 of 2003 (FCA) with the object of enhancing the welfare of the people of Tanzania by promoting and protecting effective competition in markets and preventing unfair and misleading market conducts throughout Mainland Tanzania.

Pursuant to Section 65 (2) (g) of FCA read together with Rules 41 (6), 42 (5) and 49 of the Competition Rules 2018, FCC is mandated to investigate, inter alia, entry into and exit from markets. Pursuant to Rule 33 of the Competition Rules, 2018:

RIPOTI MAALUMU

# Uuzaji kiwanda waliza serikali na wakulima

• **Miezi** 14 hakijazalisha, njaa kuanzia shambani hadi kwa mwendesha bodaboda... *Endelea ukurasa 9 & 22*

**MICHEZO** **YANGA: NAFASI ROBO FAINALI CAF BADO IPO** UK.24 **KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Samia ahamisha tena mawaziri

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya miezi minne, Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko madogo tena katika Baraza lake la Mawaziri:

Innocent Bashungwa na Dk. Damas Ndumbaro ni miongoni mwa mawaziri wanaoongoza kusimamia wizara nyingi tangu Rais Samia aingie madarakani Machi 19, 2021.

Miongoni mwa wizara alizohudumu Bashungwa ni za Ujenzi, Biashara na Viwanda na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Jerry Silaa, aliyewahi kuhudumu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na sasa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naye ameguswa katika mabadiliko hayo.

Sekta ya Habari ambayo ilikuwa sehemu ya wizara anayosimamia Silaa, imerejeshwa ilikokuwa wakati wa uongozi wa Rais Jakaya Kikwete -- Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mawaziri wengine walioguswa ni Dk. Ashatu Kijaji, ambaye amewahi kuhudumia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha na Mipango, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na sasa ameteuliwa kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mwingine ni Dk. Damas Ndumbalo, ambaye alianzia Wizara ya Katiba na Sheria, kisha Maliasili na Utalii; Michezo, Sanaa na Utamaduni na sasa amerejeshwa tena Wizara ya Katiba na Sheria.

Katika uteuzi huo, pia kuna sura mpya hasa katika nafasi ya ubalozi, wamo waliotolewa kwenye majukumu yao ya awali na kutakiwa kupangiwa kazi nyingine.

Rais Samia pia ameunda Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, sekta hiyo ikiondolewa kutoka iliyokuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Katika hilo, Rais Samia amemteua Prof. Palamagamba Kabudi, kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamad Yusuph Masauni ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Prof. Kabudi alirejeshwa kwenye uwaziri Agosti 14 mwaka huu na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Wengine walioteuliwa ni Abdallah Ulega anayekuwa Waziri wa Ujenzi, akichukua nafasi ya Bashungwa aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Gerson Msigwa, amerudishwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, lakini akiongezwa jukumu lingine la kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali.

Dk. James Kilabuko, ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Stephen Nindi ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo anayeshughulikia masuala ya ushirika na umwagiliaji wakati Dk. Suleiman Serera amehamishwa kutoka Wizara ya Kilimo kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda Biashara.



Prof. Mohamed Janabi ameteuliwa kuwa Mshauri wa Rais - Masuala ya Afya na Tiba ambaye pamoja na nafasi hiyo ataendelea kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Balozi Dk. John Stephen Simbachawene atapangiwa kituo cha kazi, Anderson Mutatembwa, Mobhare Matinyi, Kamishna wa Polisi Zanzibar CP Hamad Khamis Hamad, Kamishna wa Polisi CP Suzan Kaganda pamoja na aliyekuwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba wameteuliwa kuwa mabalozi na watapangiwa vituo vya kazi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ikulu jana, uapisho wa viongozi walioteuliwa, utafanyika Ikulu ndogo Zanzibar kesho Desemba 10.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TANZANIA), Edwin Soko, alisema wanabariki uteuzi katika Wizara ya Habari na kwamba lengo kuu ambalo wao wanataka kama wanatasnia ni kuona matokeo na Sekta ya Habari isimezwe inapowekwa katika wizara fulani.

"Cha msingi ni kuona matokeo yawe vipi. Je, inasimamia uhuru wa habari, tuna sheria rafiki, ikizungumza au wanatasnia wakizungumza inaguswa, ina matokeo yapi kila eneo?" alisema Soko.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, alisema awali wadau waliomba Sekta ya Habari ihamishwe kutoka Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ndipo ikapelekwa Mawasiliano kwa kuwa ilimezwa na mawaziri wengi kuipa kisogo.

"Rais imempendeza kuirejesha kule pa awali, tunaamini waliopewa dhamana hawataiweka kando Sekta ya Habari kama ilivyokuwa awali. Faraja tuliyoipata ni kwamba viongozi wakuu wote walioteuliwa ni wanahabari," alisema.


The Guardian Limited

VACANCY

Sales Freelancers

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales Freelancer to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, ( Moshi, Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mwanza and Zanzibar)**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

182777

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15th December, 2024.**


# ACT yakimbilia mahakamani kupinga uendeshaji Uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Said Hamdani,** LINDI

UONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo umesema hauko tayari kutambua matokeo yote ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kikidai ulijaa hila na uamuzi wa wananchi kutoheshimiwa.

Kauli hiyo ya chama ilitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Isihaka Mchinjita katika mkutano wa hadhara na wananchi uliofanyika viwanja vya Kituo cha Afya Lindi Mjini na kuhudhuriwa na maelfu ya wakazi wake.

Mchinjita alisema kuwa kutokana na mwenendo mbaya uliofanyika katika uchaguzi huo, wameamua kwenda mahakamani kupinga matokeo hayo yaliyowapa ushindi mkubwa wagombea kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mchinjita alisema uongozi wa chama umewasiliana na wanasheria kwenda mahakamani kufungua kesi kupinga matokeo hayo yaliyotangazwa na Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI kwa madai kuwa ulijaa hila nyingi dhidi ya uamuzi wa wananchi.

Alisema kwa Mkoa wa Lindi wanasheria watakaohusika ufunguaji na uendeshaji kesi husika wanatarajia kuwasili mjini kesho Jumanne Desemba 10.

"Kwa upande wetu ACT Wazalendo tunasema hatuyatambui matokeo yote ya Uchaguzi Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu," alisema Mchinjita.

Alisema hivi sasa wanaendelea kuwasiliana na vyama vingine vya siasa kujadili mwenendo mzima wa uchaguzi na hatua watakazochukua.

Aliwaomba wananchi ambao mitaa yao imekumbwa na kadhia ya kunyang'anywa ushindi kutowapa aina yoyote ya ushirikiano wenyeviti waliotangazwa washindi, huku akiwasisitiza kujitokeza kwa wingi mahakamani pale kesi ya kupinga matokeo hayo zitakapokuwa zinaendelea.

Katibu wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Lindi, Abdallah Stephen, alisema katika mitaa 117 iliyomo ndani ya Manispaa ya Lindi, wenyeviti waliopewa katika uchaguzi huo ni wanne pekee.

**Kwa maoni; +255 677 020 701**
**Email; costumerrelations@guardian.co.tz**

## HABARI KITAIFA

### MAUAJI OFISA WA TRA

# Mwigulu aungana na wanaochukua hatua

**Na Grace Gurisha**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba amesema si jambo zuri kushabikia uhalifu, akiwataka watanzania kuwa makini wasiingie katika mtego ambao maadui zao wanataka waingie wa kuvuruga na kujichukulia hatua mkononi.

Dk. Nchemba alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kuuaga mwili wa aliyekuwa mtumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Amani Simbayao aliyepigwa mawe na hadi kupoteza maisha na baadhi ya wananchi wakati akitimiza majukumu yake eneo la Tegeta kwa Ndevu, Dar es Salaam.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba

"Hili ni jambo baya pamoja na kwamba binadamu yeyote njia yetu ni moja -- ya kuonja umauti, lakini hii njia ya kulazimisha ni jambo baya kwa sababu yoyote ile, ni jambo ambalo halikubaliki nchini! Poleni sana, hili linapaswa kulaaniwa na mtanzania yeyote mpenda mema ya nchi yetu," alisema Dk. Nchemba.

Alisema watumishi hao walijitambulisha kuwa ni maofisa wa TRA, si vitu vizuri kushabikia uhalifu. Hayo si mambo ya kushabikia, hivyo analaani kitendo hicho na kuagiza hatua kali zichukuliwe dhidi ya watu waliohusika.

"Mwenzetu aliyeshambuliwa kwa mawe alikwenda kufanya jukumu alilotumwa na taifa lake la kukusanya mapato. Amani amekufa kishujaa akitimiza majukumu yake, tuache kufuata mkumbo," alionya Dk. Nchemba.

Pia alisema kitengo cha kupambana na magendo alichokuwa anafanya Amani, na mazingira ya kifo chake, kinatoa ukumbusho kwa maofisa hao kukatiwa bima ili wawe na uhakika kwa sababu ni kitengo kichohusika na kazi ngumu.

Dk. Nchemba alisema anaunga mkono alichokizunguza mkuu wa mkoa cha kuwanunulia hatifungani watoto wa marehemu katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ili awasaidie katika maisha yao, mfuko huo uanzishwe na waanze kwa kuchangia Sh. milioni 200.

"Nitawachukua watoto wa marehemu hadi pale haya yote yatakapokamilika ili tuweze kumuenzi shujaa wetu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alisema, "Kuuawa kwa Amani ni hasara, haina mbadala, hatuwezi kusema Amani atapata mbadala kwenye dunia hii, tushapigwa hasara kubwa sana kwa taifa na familia yake.

"Amani amefungua ukurasa mpya kwenye utawala wangu kama Mkuu wa Mkoa na lazima huo ukarasa lazima ujibu na lazima ulete mashahidi... lazima damu iliyomwagika itabeba, lazima eneo litokea tukio patasafishwa na nikisema patasafishwa patasafishwaje, sijawahi kuwa kiongozi legelege kwenye mambo ya msingi, siku zote ninabeba uamuzi mzito."

Kamshna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda alisema watumishi wa TRA ambao ni kikosi cha ukusanyaji kodi, watapewa ulinzi wa Jeshi la Polisi ili kuhakikisha usalama wao.

"Kama ambavyo tumekubaliana kuwa hatutatumia nguvu kwenye kusimamia kodi, tutaendelea hivyo lakini kwa kile kitengo cha 'Fast' ambacho kinapambana na walioamua kukwepa kodi, kuanzia sasa hatutawaacha wafanye kazi pekee yao, watafanya wakiwa na polisi," alisema.

Alisema Amani amefariki dunia kwa kushambuliwa kipindi ambacho anatimiza majukumu yake ya kusaidia nchi hii na wananchi wote.

"Alichotendwa hakustahili kutendwa. Sisi tunalaani vikali sana, wale wote waliochukua sheria mkononi kinyume cha sheria hapakuwa na sababu yoyote inayohalalisha kufanya walichofanya, alikuwa anafanya kazi zake kwa mujibu sheria," alisema.

***Kwa maoni; +255 677 020 701***
***Email; costumerrelations@guardian.co.tz***






TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI
BODI YA MFUKO WA BARABARA

# HERI YA SIKUKUU YA UHURU

## 09 DISEMBA 2024

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote, katika kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

*"Uongozi Madhubuti na Ushirikishwaji wa Wananchi ni Msingi wa Maendeleo Yetu"*



#KAZIIENDELEE

**Barua pepe:** info@roadsfund.go.tz **Tovuti:** www.roadsfund.go.tz @mfukowabarabara

@bodiyamfukowabarabara @rfbtz

# Miaka 63 ya Uhuru na Hali ya Mtandao wa Barabara Nchini

Mtandao wa barabara hapa nchini una jumla ya **kilometa 181,602.2** zikijumisha **kilometa 37,225.7** za barabara za Kitaifa na **kilometa 144,376.5** za barabara za Wilaya. Barabara za Kitaifa zinasimamiwa na TANROADS na barabara za Wilaya zinasimamiwa na TARURA.

Kutokana na hali ya jiografia ya nchi yetu, usafiri wa barabara ndiyo njia inayotumiwa zaidi kwa usafiri na usafirishaji. Inakadiriwa kuwa zaidi ya **asilimia 90 na 80** ya abiria na mizigo, mtawalia, hutumia barabara.

Hivyo ufanisi wa mipango ya Serikali inayolenga maendeleo ya vijijini, uzalishaji wa ajira, maendeleo ya viwanda, kwa kiasi kikubwa, unachangiwa na ubora wa huduma za usafiri wa barabara.

Aidha, miundombinu ya barabara ndiyo rasilimali ya umma yenye thamani kubwa zaidi. Thamani yake inakadiriwa kufikia Shilingi Trilioni 39.5 - sawa na asilimia 23 ya Pato la Taifa.



*Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Barabara Mhandisi Rashid Kalimbaga*

## Uboreshaji wa miundombinu ya barabara

Kwa kutambua thamani na umuhimu wa barabara kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Serikali imekuwa ikiimarisha uwezo wa kifedha na kitaasisi ili kuzilinda barabara kwa lengo la kuziwezesha kutumika kwa muda uliopangwa. Serikali imekuwa ikitenga **Shilingi bilioni 850** kila mwaka kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara hapa nchini. Fedha hizi zimewezesha utekelezaji wa wastani wa **miradi 620** ya matengenezo ya barabara kwa barabara za Kitaifa na **miradi 850** kwa barabara za Wilaya kila mwaka.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikiimarisha uwezo wa taasisi zinazosimamia kazi za barabara, hususan TANROADS, TARURA na Bodi ya Mfuko wa Barabara, kwa kuziongezea vitendea kazi pamoja na wataalam.

Kutokana na kufanyika kwa matengenezo hayo, zaidi ya **asilimia 90** ya mtandao wa barabara za Kitaifa uko kwenye hali nzuri na wastani. Aidha zaidi ya **asilimia 60** ya mtandao wa barabara za Wilaya uko kwenye hali nzuri na wastani. Hivyo sehemu kubwa ya mtandao wa barabara unapitika kipindi chote cha mwaka. Hali hii imeiwezesha Tanzania kuwa moja ya nchi za Afrika zenye mtandao bora wa barabara ambao sehemu kubwa inapitika majira yote.

Hata pale mawasiliano ya barabara yanapokuwa yamekatika kutokana na mafuriko, Serikali imekuwa ikitoa fedha mara moja ili kurudisha mawasiliano kwa wakati na hivyo kuwawezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Mfano ni kazi za dharura zilizofanyika maeneo ya Hanang (Manyara), Liwale (Lindi) na Ununio (Dar es Salaam).

Kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara, wananchi wamewezeshwa kuzifikia kwa urahisi huduma za kijamii na kiuchumi kama vile elimu, afya, masoko, ajira na fursa nyingine za kujipatia kipato.

Tunachukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mkazo katika kuimarisha miundombinu ya barabara na hivyo kuiwezesha kutoa mchango unaotarajiwa kwenye maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Bodi ya Mfuko wa Barabara itaendelea kufanya kazi kwa juhudi na umahiri ili kutoa mchango unaotarajiwa ili kufikia malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita.



*Muonekano wa Daraja la Ngira mkoani Kilimanjaro lililojengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya awamu ya sita zaidi ya madaraja 160 yamejengwa kwa kutumia teknolojia mbadala ya mawe na matofali ya kuchoma. Madaraja haya ni imara na yanauwezo wa kupitisha magari yenye uzito wa hadi tani 40.*

## Usimamizi na ugharamiaji wa matengenezo ya barabara

Barabara zikishajengwa uhitaji kufanyiwa matengenezo kikamilifu ili kulinda thamani yake, uwekezaji wa Serikali na kuziwezesha kutumika kwa muda uliopangwa. Hii ni kwa sababu ubora wa barabara hupungua kutokana na kuzeeka, uzito wa magari na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Matengenezo yasipofanyika kikamilifu, barabara uharibika mapema na hivyo kupoteza thamani yake, thamani ya uwekezaji wa Serikali na kuongeza gharama za usafiri na usafirishaji.

Matengenezo ya barabara hapa nchini yanasimamiwa na kugharamiwa chini ya **Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura 220.** Chini ya Sheria hii, Serikali iliunda **Mfuko wa Barabara na Bodi** yake mwaka 2000 ili kuhakikisha uwepo wa kutosha na endelevu wa fedha za kugharamia matengenezo ya barabara. Serikali ilianzisha Mfuko wa Barabara kama moja ya mifuko maalum chini ya **Ibara ya 135(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Serikali ilianzisha Mfuko na Bodi yake kama njia ya kutatua changamoto kubwa ya ubovu wa mtandao wa barabara kati ya miaka ya 1980 na 1990 kutokana na kutofanyiwa matengenezo kikamilifu. Nchi nyingi za Afrika zilianzisha mifuko ya aina hii na hadi sasa kuna nchi 34 zenye mifuko hiyo.

Kwa mujibu wa Sheria, majukumu makuu ya Bodi ni kuhakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha za kugharamia matengenezo, kugawa fedha hizo kwa Wakala za Barabara na kufuatilia matumizi ya fedha hizo.

Tozo ya mafuta ni chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko kwani huchangia wastani wa asilimia 96 ya mapato yote ya Mfuko. Tozo ya mafuta kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara ni TZS 263 kwa kila lita ya petroli na dizeli. Vyanzo vingine ni ushuru wa magari ya kigeni (transit charges) na Tozo ya uzidishaji wa uzito.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Barabara na Mafuta, Sura ya 220, makusanyo yote ya Mfuko wa Barabara yanatakiwa yawekwe kwenye akaunti ya Mfuko wa Barabara inayosimamiwa na Bodi. Hii ni kwa sababu mapato hayo yametengwa mahsusi (ring-fenced) kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara za Kitaifa na Wilaya zinazosimamiwa na TANROADS na TARURA, mtawalia.

Moja ya mafanikio makubwa ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Barabara na Bodi yake ni kuimarika kwa ubora wa mtandao wa barabara hapa nchini. Barabara za Kitaifa zilizo kwenye hali nzuri zimeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 90 kutoka wastani wa asilimia 13 mwaka 2000. Aidha, barabara za Wilaya zilizo kwenye hali nzuri na wastani zimeongezeka na kufika asilimia 60 toka asilimia 10 mwaka 2000.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kamati ya Waamuzi tujuzeni sasa hatima suala la Kayoko

**BAADA** ya kuchezesha mechi ya dabi ya Simba na Yanga, Oktoba 19, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, iliyokuwa na maamuzi mengi yenye utata, mwamuzi Ramadhani Kayoko hajaonekana tena uwanjani.

Hajaonekana kuchezesha mechi yoyote kitu ambacho si cha kawaida, kwani inakaribia miezi miwili sasa, kwa mwamuzi kama yeye angekuwa angalau tumemwona akichezesha walau hata mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika mchezo wa Oktoba 19, ambao Yanga ilishinda bao 1-0, kulikuwa na maamuzi mengi ya kufikirisha, ambapo kwa mujibu wa baadhi ya viongozi wa Simba, wachambuzi, pamoja na marudio ya video, kulikuwa na matukio ya mchezaji Kibu Denis kuangushwa mara tatu ndani ya eneo la hatari.

Hakutoa walau penalti moja, pamoja na matukio mengi ambayo viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba walilalamika kuwa walinyongwa na mwamuzi huyo.

Siku chache baadaye, waliojiita kama wazee wa Simba walijitokeza na kulalamika kuwa kulikuwa na mchezo mchafu, au mipango ovu dhidi ya timu yao iliyowashirikisha baadhi ya vigogo nchini, wakidai kumshinikiza mwamuzi huyo achezeshe kwa kuidhoofisha timu yao kwenye mchezo huo.

Wazee hao walidiriki hata kutoa mifano na kusema kama iliwezekana wanaweza kuwataja watu ambao walimshinikiza mwamuzi huyo.

Hata hivyo, wiki chache baadaye, Kamati ya Uendeshaji ya Bodi ya Ligi, ilikutana ambapo pamoja na mambo mengine ilisema suala la Kayoko na waamuzi wenzake, limepelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu ya Waamuzi baada ya kuonekana kutoutendea haki mchezo huo wa dabi.

Ilikuwa ni mwanzoni mwa Desemba ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi, Nassor Hamduni, alipothibitisha kuwa shauri la mwamuzi huyo limepelekwa kwenye kamati hiyo kwa ajili ya kujadiliwa na wajumbe wa kamati hiyo na kutoa ushauri wa kitaalamu kabla ya kufanyiwa maamuzi.

Ni mwezi mmoja sasa, hatujasikia lolote kuhusu mwamuzi huyo, kitu ambacho kinatufanya tuhoji kuhusu maamuzi ya kamati hiyo na kama ameadhibiwa basi isiwe kimya kimya ili kuwafanya na wengine kuchukua tahadhari kwa kuongeza umakini wanapopewa dhamana ya kuchezesha mechi.

Kwa hali ya kawaida, kama mchezaji amefanya kosa lolote ambalo linahitaji Kamati ya Nidhamu na Hadhi za Wachezaji ikae, mchezaji anaendelea kucheza hadi maamuzi yatakapotolewa, kama atakuwa hajaadhibiwa kwa kadi ya njano au nyekundu ya uwanjani.

Na hata waamuzi wengine huwa hawasimamishwi, badala yake wanaendelea kuchezesha hadi pale kamati itakapotoka na maamuzi ndipo anapoanza kutumikia adhabu yake.

Kwa Kayoko sivyo, kwani hajaonekana tena kuchezesha mechi yoyote, huku suala lake likiwa kwenye Kamati ya Waamuzi.

Hii haimtendei haki hata yeye mwenyewe ambaye hajui hatma yake itakuwa nini na lini. Ni wakati sasa wa kamati husika kutoka na kuweka wazi kama ni kuadhibiwa itangaze na yeye kuanza kutumikia adhabu yake lakini pia kutoa fundisho kwa wengine wanaochezesha chini ya kiwango.


Kumuondoa kwenye ratiba kimya kimya, si sahihi kwani hakutatoa nafasi kwa wengine kutambua wakifanya makosa adhabu wataadhibiwa kwa kiwango gani, ili kuchukua tahadhari.

Lakini hivi kweli tumefika mahali sasa mambo yanakwenda kimya kimya mpaka wadau hatuelewi nini kinaendelea kwa suala la Kayoko?

Je, wakubwa wanaogopa maswali? Wanaogopa kusema alikosea nini? Kuogoka kuongea suala hili au kutoa maamuzi kunawafanya wadau wa soka kufiriki na wao ni sehemu ya makosa yake. Labda sasa watuambie pia kuna kanuni ya kuadhibiwa kimyakimya? Ili nasi tujue.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Nafasi ya Yanga robo fainali michuano ya CAF hii hapa

Na Adam Fungamwango

**KIPIGO** cha mabao 2-0 ilichokipata Yanga juzi dhidi ya MC Alger ya Algeria, kimewafanya baadhi ya mashabiki wao kuanza kukata tamaa ya kupita hatika hatua ya makundi.

Baada ya mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Julai 5 jijini Algiers, mashabiki wengi waliokuwa wakiangalia kwenye televisheni na hata ukisoma kwenye mitandao ya kijamii, wanaonekana kukata tamaa kuwa inawezekana msimu huu timu yao isiweze kupita hatua ya makundi na kwenda robo fainali kama ilivyokuwa msimu uliopita, ilipotolewa hatua hiyo kwa mikwaju ya penalti 3-2 dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, baada ya suluhu katika michezo yote miwili ya nyumbani na ugenini.

Sababu kubwa ni kipigo cha pili mfululizo ilichokipata kwenye michuano hiyo, cha kwanza ikikipata nyumbani dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, ikichapwa pia mabao 2-0.

Nadhani hawaoni mwanga tena mbele, kwani katika michezo hii, malengo makubwa ya timu zinazotaka kupita makundi ni kushinda mechi zote tatu za nyumbani kwanza. Inawezekana kabisa pointi hizo zinakufanya kupita kwa kushika nafasi ya pili, lakini pia zipo timu zinashinda ugenini au kupata hata pointi moja.

Mfano Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema lengo ni kupata pointi 10, ambazo mpango wake ni kuzipata tisa nyumbani na moja kuipata katika mechi tatu za ugenini ambazo zitamwezesha kusonga mbele.

Haya ndiyo mahesabu ya michuano hii ya kimataifa kwa timu ambazo ziko 'siriasi' hasa.

Yanga imepoteza mechi moja nyumbani na moja ugenini. Kwa maana hiyo, mahesabu yake sasa ni kushinda michezo yote mwili ya nyumbani ili kupata pointi sita kwanza.

Halafu ishinde mechi moja ugenini na moja sare katika michezo miwili ya ugenini iliyobaki. Kwa baadhi ya mashabiki wa Yanga wanaona kama itakuwa ngumu kutokana na mwenendo wao kwa siku za karibuni hata kwenye michezo ya Ligi Kuu.

Niwatoe wasiwasi wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa wasikate tamaa timu hiyo inaweza kuvuka hatua hii kama mikakati thabiti itapangwa.

Wasiwasi ni kwamba wanachama na mashabiki wa Yanga wanaweza wasijitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenda kuisapoti timu yao, kitu ambacho hawatakiwi kufanya hivyo kwani nafasi bado wanayo ya kusonga mbele.

Mara nyingi hawana tabia ya kwenda kujazana uwanjani kama timu yao inafanya vibaya. Hii inaweza kufifisha juhudi za viongozi na wachezaji kutinga hatua ya robo fainali.

Kinachotakiwa kwa wanachama na mashabiki wa Yanga, hajjalishi timu inapitia kipindi kigumu liasi gani, lakini inatakiwa kujazana uwanjani ili kuipa nguvu.

Ikumbukwe kuwa Simba ilipitia kipindi kigumu kama hicho, mfano tu msimu uliopita, ilitoka sare ya bao 1-1 nyumbani dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, suluhu ugenini dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, baadaye ikafungwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco.

Hapa utaona kuwa kwenye michezo mitatu ilikuwa haijashinda hata mchezo mmoja, lakini ikapambana na kushinda mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Wydad Casablanca, kabla ya kulazimishwa suluhu kwa mara nyingine dhidi ya Asec Mimosas ugenini.

Hii inaonesha kuwa Simba ilipita kwenye njia ngumu mno, kiasi kwamba mechi mbili za mwisho ililazimika kushinda zote, ikaifunga Jwaneng Galaxy mabao 6-0 na kutinga hatua hiyo.

Misimu mwili iliyopita kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba baada ya kupoteza michezo miwili mfululizo, ilionekana kama imeshatolewa kwenye kinyang'anyiro cha kutinga robo fainali kwa kushika nafasi ya mwisho kwenye kundi, lakini ilishinda michezo miwili mfululizo dhidi ya Vipers ya Uganda na kurejesha matumaini, kabla ya mchezo wa mwisho kuikandamiza Huroya mabao 7-0, ikatinga kwa kishindo robo fainali.

Mifano hii ni kuonesha kuwa Yanga kama itakaa chini na kupiga hesabu zake vizuri, kuandaa mikakati ya ndani ya uwanja ya kiufundi ikichanganya na rasilimali watu ambao ni mashabiki wake kwa kuwahamasisha kujazana uwanjani kwenye kuipa sapoti, kama ilivyokuwa ikifanya Simba huko nyuma, ikipita mara kwa mara katika mazingira magumu, basi hakuna kitakachoshindikana kwa kutinga robo fainali.

## HABARI KITAIFA

# Mgombea upinzani ashinda urais Ghana

**ACCRA,** Ghana

KIONGOZI wa chama cha upinzani cha National Democratic Congress (NDC), John Mahama ambaye alikuwa rais wa nchi hiyo kutoka 2012 hadi mapema 2017, ameibuka mshindi katika nafasi ya urais kwenye uchaguzi uliofanyika jana.

Kiongozi huyo amemshinda Makamu wa Rais wa nchi hiyo, Mahamudu Bawumia aliyekuwa akiwania nafasi hiyo kupitia chama tawala cha New Patriotic Party (NPP).

Ushindi huo umetokana na zaidi ya wananchi milioni 18 wa Ghana walioshiriki kupiga kura katika uchaguzi mkuu nchini humo na kumchagua mrithi wa Rais Nana Akufo-Addo, ambaye anaachia ngazi baada ya kuitumikia mihula miwili.

Katika uchaguzi huo ambao ulifanyika juzi, wananchi pia waliwachagua wawakilishi wapya katika bunge la nchi hiyo.

Katika uchaguzi huo wagombea 11 wa vyama tofauti walijitokeza, na matokeo yalianza kutangazwa baada ya uchaguzi kumalizika na kura kuhesabiwa.

Ghana ina historia ya utulivu wa kisiasa, vyama viwili vikuu vya NPP na NDC vimepishana madarakani kwa amani tangu nchi hiyo iliporejesha demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992.

Wizara ya Mambo ya Ndani ilisema serikali ya Ghana ilifunga kwa muda mipaka yote ya ardhini tangu Ijumaa usiku hadi jana ili kuhakikisha mchakato wa kura unaendelea vizuri. **AFP/AP/DW**



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Salim Msangi, akizungumza na waandishi wa habari juzi kuhusu maadhimisho ya Siku ya Usafiri wa Anga Duniani pamoja na kuwapongeza vijana wa kitanzania waliobahatika kupata udhamini wa kusomea urubani na uhandisi wa ndege Makao Makuu ya Mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: TCAA**

# Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

**Na Tuntule Swebe**

MTOTO Joshua Tarimo (11) ametoweka nyumbani kwa mlezi wake Tandale Kwatumbo, Dar es Salaam tangu Desemba 5, mwaka huu.

Mlezi wa mtoto huyo, Salama Salimu, akizungumza na Nipashe jana alidai kuwa mwanawe huyo alitoweka Desemba 5 mwaka huu asubuhi.

"Niliangalia fedha zangu mahali ninapoweka sikuziona. Baada ya kufuatilia kwa kina, nilihisi mwanangu ndiye kazichukua, nilimwuliza mwanangu aitwaye Asma Mohamed (21) na Joshua.

"Katika kuwahoji ilibainika Joshua ndiye kazichukua fedha hizo na kumtaka azirudishe, ndipo aliamua kuondoka kwenda kusikojulikana kwa kuhofia kupewa adhabu.

"Saa chache ndipo nilipogundua kuwa Joshua hayupo nyumbani, nilimtafuta sikumpata ndipo nilipochukua jukumu la kumwambia mama yake.

"Nilipojaribu kumwuliza mama yake, alisema mtoto huyo hakuwa kwake, tulimtafuta kwa ndugu wa karibu, lakini hatukumpata," alisema.

Salama alisema wameshatoa taarifa kituo cha polisi na kufungua faili namba MBT/RB/6328/2024.

"Ninaogopa sana huyu mwanangu asikumbwe na jambo baya, kwa sasa kuna matukio ya watu kupotea na kutekwa, nina hofu sana, kokote aliko arudi nyumbani," alisema.

Alisema kuwa siku hiyo alikuwa amevaa fulana ya rangi ya chungwa na suruali ya rangi ya kijivu na yeboyebo za rangi ya kijani. Atakayemwona awasiliane na mama huyo kwa namba 0684304142 au 0719058662.








CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
C.W.T
WAJIBU NA HAKI
MAADHIMISHO YA MIAKA 63 YA UHURU
(1961 - 2024)
COMPLETE INDEPENDENCE 1961
UONGOZI WA CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT) WANAUNGANA NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, KATIKA KUSHEREHEKEA MAADHIMISHO YA MIAKA 63 YA UHURU WA TAIFA.
1961 - 2024
MH. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
218289102

**RIPOTI MAALUMU**

# Uuzaji kiwanda waliza serikali na wakulima



Mkulima wa chai, karibu na eneo la kiwanda hicho, aliyekutwa shambani na mwandishi wa habari hii mwezi uliopita, akichuma chai iliyokomaa kupitiliza baada ya kukosa soko kutokana na kiwanda hicho kufungwa. **PICHA: HALFANI CHUSI**

**Na Halfani Chusi aliyekuwa** LUSHOTO

KIWANDA cha chai cha Herkulu Estate katika Halmashauri ya Bumbuli wilayani Lushoto mkoani Tanga kimesitisha uzalishaji kwa mwaka mmoja na miezi miwili sasa:

Wakulima wa chai katika halmashauri hiyo wanaokitegemea kiuchumi, wako njiapanda; kuna waliokata tamaa ya kuendelea kulima, wameng'oa miche ya chai na kupanda miti ya mbao; wengine wanalia wamekosa ajira kiwandani na wengine wanalalama wameshindwa kumudu mahitaji ya familia.

Pia wanalalama mzunguko wa fedha umekuwa mgumu kwao; bodaboda sasa hawana uhakika wa kupata abiria na baadhi ya wanafunzi wamelazimika kukatisha masomo kutokana na wazazi/walezi kushindwa kumudu mahitaji ya shuleni.

Ni vilio vinavyosikika katika eneo hilo baada ya kampuni ya Bombay Burmah Trading Cooperation Limited (BBTCL), wamiliki wa Herkulu Estate, kuamua kuuza kiwanda hicho kwa kampuni ya Udongo Wetu Limited ya Dar es Salaam.

Mhasibu Mkuu wa Kiwanda hicho, Eliezer Jengo, amemweleza mwandishi wa habari hii kuwa BBTCL, yenye makao makuu yake katika mtaa wa Wallace, Fort, jijini Mumbay, India, ilishasitisha uzalishaji katika kiwanda chao tangu Septemba mwaka jana. Hivyo, leo ni mwaka mmoja na miezi miwili kiwanda hakizalishi. Kiwanda kilianza rasmi uzalishaji mwaka 1955, yaani miaka 69 iliyopita.

Udongo Wetu Limited, waliouziwa kiwanda hicho Septemba mwaka jana, hawajaanza uzalishaji. Kwa nini? Mhasibu Mkuu wa kampuni hiyo, Nasri Hussein, amemwambia mwandishi kwamba hawajapata kibali cha Tume ya Ushindani (FCC) kuendeleza uzalishaji kiwandani huko.

Matokeo yake, wakazi wa Bumbuli na maeneo jirani, waliotegemea kiwanda hicho kuendesha maisha yao, sasa wamekosa mahali pa kupata ujira na soko la chai yao.

Kwa mujibu wa Mhasibu Mkuu Jengo, wakati wa uzalishaji kiwandani, BBTCL walipokea wastani wa tani 10 za majani ya chai kwa siku na ulipotimia msimu wenyewe wa mavuno ya chai (Septemba hadi Machi) walielemewa na malighafi, wazalishaji wakuu wakiwa ni wakazi wa Bumbuli na maeneo jirani.

Anafafanua kuwa kulingana na uzoefu wake kiwandani, tani 10,000 za majani ya chai walizokuwa wananunua kwa siku, zilikuwa zinatoa kilo 2,500 za bidhaa (chai yenyewe).

Kukiwa na kilio hicho kwa wakulima wa Bumbuli, Wizara ya Kilimo inabainisha kuwa uzalishaji chai nchini ulishuka kwa asilimia 49.5 mwaka 2023/24 kulinganisha na mwaka uliotangulia.

Katika hotuba yake bungeni Juni 11 mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alibainisha kuwa uzalishaji chai ulifikia tani 13,525 mwaka 2023/24 kulinganisha na tani 26,753 mwaka 2022/23 sawa na asilimia 45 ya lengo la kuzalisha tani 30,000 mwaka 2023/24.

Hii ina maana kwamba uzalishaji chai nchini umeshuka kwa asilimia 50.5 mwaka 2023/24 kulinganishwa na uzalishaji wa mwaka uliotangulia (2022/23).

Mkulima wa Chai na Mkazi wa Bumbuli, Ramadhani Sharifu anasema kiwanda hicho kusitisha uzalishaji kumewayumbisha kiuchumi, wengi wao sasa wamehamia rasmi kwenye maisha magumu, kilio cha maisha magumu kimeanza kuwa msamiati wa kawaida kwa wenyeji.

"Wapo wanaotegemea kiwanda hiki kwa ajili ya kusomesha watoto wao, kupata fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula na kumudu mahitaji mengine ya kijamii, lakini sasa hakifanyi kazi," analalama mkulima huyo ambaye alikutwa shambani akikata baadhi ya miche ya chai na kupanda miti ya mbao.

Mkazi mwingine wa Bumbuli, Hassan Ramadhani anaungana na mkulima mwenzake Sharifu kupaza sauti dhidi ya adha wanayopita hivi sasa. Anasema hawana soko kwa ajili ya chai yao baada ya kiwanda hicho kusitisha uzalishaji.

Anasema baadhi ya wakulima wamekata tamaa kutokana na kupata hasara. Matumaini yao pekee -- ipo siku serikali itaingilia kati suala hilo, hata kiwanda kurejea katika uzalishaji na wao kupata mahali sahihi pa kuuza chai yao kama ilivyokuwa awali.

"Wakulima wengi wamewekeza katika zao hili na wanategemea kilimo hiki cha chai. Soko linapokosekana na mzigo (bidhaa) upo wa kutosha, inakatisha tamaa kabisa. Na hiki kinachotusibu sisi hapa Bumbuli ni kinyume

INAENDELEA UK.22


bgtl **BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI YA SIKU 14/MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **NCBA Bank Tanzania Limited** tunatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa tajwa hapo chini kwenye jedwali alipe deni analodaiwa na banki Pamoja na riba. Kushindwa kufanya hivyo mali iliyowekwa kama dhamana itauzwa Kwa njia ya mnada wa hadhara kufidia deni hilo.Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo tarehe na muda kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA /MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|---|
| 1 | ELI TUNU MALAMIA | NYUMBA YA MAKAZI YENYE HATI NA. 49176 KIWANJA NA. 130 KITALU "B" ENEO LA TEGETA MANISPAA YA KINONDONI YENYE JINA LA ELI TUNU MALAMIA | 16-01-2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ 765 363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NCBA Bank Tanzania Limited**
**P. O. BOX 20268, DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 22 2130113 / 255 22 2125710**

218290802



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA ARUSHA, KILIMANJARO NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA CHEMBA, KONDOA NA MJI WA KONDOA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dodoma katika Halmashauri za Wilaya za Chemba, Kondoa, na Mji wa Kondoa kuanzia tarehe 11 hadi 17 Desemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 11 hadi Jumanne tarehe 17 Desemba, 2024.
2. VITUO: Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua namba 3 (Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 03 Desemba, 2024 na:

**Livini A. Morrice**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**



# TASHICO: Usafirishaji njia ya majini ni nafuu, salama

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKURUGENZI wa Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO), Eric Hamiss, amesema kusafirisha bidhaa kwa njia za majini ni nafuu zaidi na salama kuliko njia nyingine, kutokana na urahisi uliopo na uwekezaji uliofanyika katika sekta hiyo.

Alibainisha hayo juzi wakati akiongea na Nipashe na kueleza kuwa uwekezaji unaoendelea kufanywa kwenye ujenzi wa meli utaongeza biashara ya ndani na nchi jirani.

"Ujenzi wa meli za mizigo utawezesha Tanzania kuimarisha biashara na nchi jirani kama Uganda, Kenya, Zambia, Burundi, DRC na Malawi, jambo ambalo litapanua soko kwa bidhaa za ndani na kuleta fedha za kigeni," alisema Hamissi.

Alisema kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Kampala (Uganda) kwa barabara ni kilometa 1,717 lakini kutoka Dar es Salaam hadi Kampala kupitia Ziwa Victoria ni kilomita 1,470.

"Vilevile mizigo inayokwenda Kalemie, DRC ni rahisi kupita Ziwa Tanganyika kuliko kupita njia ya barabara, aidha upite Tunduma kisha Zambia km 1,922 au upitie Burundi km 1,877 lakini kutoka Dar es Salaam kwenda Kalemie (DRC) kupitia Bandari ya Kigoma ni kilomita 1,375," alisema.

Hamissi baada ya uhuru, shirika lilikuwa chini ya uangalizi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini serikali iliendelea kutoa huduma ya usafiri kwa njia ya maji katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwa kutumia meli tatu.

"Hata hivyo, serikali ilinunua meli mpya saba, ambako MSCL ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni Sura 212, Desemba 8, 1997 kutoka Shirika la Reli (TRC), lakini rasmi MSCL ilianza kazi Agosti 1, 1999 ikiwa na meli 14 na boti moja," alisema.

Aliongeza: "Mwaka 2018, serikali ilianza kutenga fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa minne katika Ziwa Victoria na mwaka 2022, serikali iliielekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kukabidhi meli tatu za Mv. Mbeya II, Mv. Njombe na Mv. Ruvuma kwa MSCL ambazo hadi sasa meli hizo zinaendelea kutoa huduma katika Ziwa Nyasa," alisema.

Alisema katika awamu ya kwanza ya miradi 2018/23 ilihusisha miradi minne mojawapo ikiwa ni ujenzi wa meli mpya ya Mv. Mwanza "Hapa Kazi Tu", yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria, pamoja na ujenzi wa chelezo.



Mwonekano wa ubovu wa barabara ya kutoka Chuo cha Ufundi Stad Veta Manispaa ya Shinyanga, kwenda Kijiji cha Lyandu katika manispaa hiyo, namna ilivyoharibiwa na mvua, huku wananchi pamoja na magari yakipata shida kupita kwenye barabara hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Balozi wa mazingira 'alia' kunyimwa ushirikiano

**Na Remmy Moka,** MWANZA

BALOZI wa mazingira kutoka ofisi ya Makamu wa Rais, Mrisho Mabanzo 'Mr. Tree' amewaomba viongozi wa taasisi pamoja na jamii kutoa ushirikiano kwa wadau wanaoweka juhudi muhimu za udhibiti wa uharibifu wa mazingira.

Alibainisha hayo juzi jijini Mwanza wakati wa mbio za kuhamasisha matumizi ya nishati safi na utunzaji mazingira kwa kupanda miti.

Alisema ikiwa kila mmoja atatekeleza jukumu lake kwa nafasi yake, itasaidia kuirahisishia serikali kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa nishati safi na mazingira salama.

Mabanzo alisema katika utekelezaji wa kazi ya ubalozi wa mazingira kuna baadhi ya viongozi wamekuwa wakimnyima ushirikiano, hali inayorudisha nyuma juhudi za serikali kufikia matumizi ya nishati safi na mazingira salama.

Ofisa kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Maija Mkomwa alisema TFS wanawajibu wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi na upandaji wa miti, ili kuifanya Tanzania iwe ya kijani kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Alisema katika kutekeleza hilo wana vitalu vya miti yenye miche ya aina mbalimbali kwa ajili ya kuigawa bure pamoja na kutoa elimu ya namna ya bora ya kuitunza na kuifadhi kwa ajili ya ulinzi wa mazingira kwa vizazi endelevu.

Mhandisi Lukas Peleka akimwakili Meneja wa NEMC Kanda ya Ziwa, alisema ikiwa kizazi cha sasa kitawekeza katika upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira itasaidia katika jamii kupata hewa inayostahiki na kujiepusha na magonjwa.

Padree Thomas Kabilingi alisema amekuwa mdau wa kuhamasisha upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira tangu mwaka 1984, ambapo alikuwa akipanda miti na kuisambaza shuleni, kanisani, mistikini na taasisi binafsi na za umma.

Hivyo, aliitaka jamii iwe na utaratibu wa matumizi ya nishati safi ili kuiweka Tanzania

# Wajomba watajwa chanzo ukatili kijinsia kwa watoto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

NDUGU wa familia wakiwamo wajomba wametajwa kuwa chanzo cha ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto.

Pia ndugu hao wamekuwa wakiwalawiti watoto ambao asilimia kubwa ni wanafunzi kisha kuyamaliza kiundugu, hali inayosababisha watoto kuathirika kisaikolojia, kushindwa kusoma ipasavyo na kutokutimiza ndoto zao za kielimu.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Robert Kwela wakati akitoa taarifa ya hali ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii na familia.

Alisema hali hiyo imebainika kutokana na utafiti walioufanya ambako walibaini wajomba kuwaingilia kwa nguvu kingono watoto wa dada zao, endapo wakibainika wanamaliza kimya kimya.

Kwela alisema wameshaweka mifumo rafiki ya kutoa taarifa ya vitendo hivyo kwa lengo la kusaidia kundi la watoto wasiendelee kufanyiwa vitendo viovu ambavyo vinasababisha kuchukia makazi yao na kukimbilia mjini kutafuta maisha wakiwa na umri mdogo, huku wanandugu watakaobainika wanawachukulia hatua za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.

"Ukatili unasababisha kuwa na ongezeko la watoto wengi wa mitaani, kwa ripoti ya Novemba mwaka huu inaonesha watoto nje ya ndoa 132 wamefanyiwa ukatili, huku walipo ndani ya ndoa wakiwa 148, watoto waliobakwa ni 60 watu wazima 16 na hakuna ushirikiano wowote zinapofika katika vyombo vya sheria huku zaidi ya watoto 36,564 wakikimbilia mitaani," alisema Kwela.

Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Kahama, Salumu Rashidi, alikiri kuwepo kwa wimbi la watoto wa mitaani kutoka Burundi na wengi wanafanyishwa kazi za ndani na biashara ndogo ndogo na kinamama.

Hivyo, aliwataka kuacha tabia hiyo kwani sheria inakataza mtoto chini ya miaka 18 kupewa majukumu ya kazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, aliwasihi wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa na kuwaibua waathirika wa ukatili ili wahusika wachukulie hatua za kisheria na kesi zinapofika mahakamani wajitokeze kutoa ushahidi na siyo kumalizana kimya kimya.

Nipashe
Spotika




WANASOKA MASHABIKI WA MPIRA WA KIKAPU NA WAKALI WA MAVAZI UK. 12



PEP GUARDIOLA

# ZAMA ZA GUARDIOLA CITY NDIO BASI TENA?

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City ambayo imeshinda Kombe la Ligi Kuu England (EPL), mara nne mfululizo chini ya Kocha Pep Guardiola, imekuwa na msururu wa matokeo mabovu kwani haijashinda katika mechi sita za mwisho ikipoteza mechi tano kati ya hizo.

Novemba 23, mwaka huu, ilicharazwa mabao manne bila jibu nyumbani dhidi ya Tottenham Hotspur, ikachapwa tena mawili na Liverpool.

Guardiola alionekana wazi amegadhabishwa kwa kutoka sare ya mabao matatu na Feyenoord baada ya timu yake kuongoza kwa mabao matatu katika kipindi cha kwanza.

Hata hivyo, Pep Guardiola, amesema wachezaji wake wanahuzuni kutokana na mfululizo wa kupoteza mechi tano, lakini ana matumaini kugeuza hali hiyo.

Kupoteza mabao 4-0 nyumbani kwa Tottenham kulikuwa pigo kubwa siku chache tu baada ya Guardiola kusaini mkataba mpya wa miaka miwili kwenye klabu hiyo.

Ilikuwa ni kipigo kikali zaidi kwa City nyumbani tangu mwaka 2003 na mara ya kwanza kupoteza mechi tano mfululizo tangu 2006, kabla ya Sheikh Mansour kuanza kipindi chake cha mafanikio makubwa kama mmiliki.

Guardiola hajawahi kupoteza mechi tano mfululizo katika kipindi chote cha kazi yake ya ukocha.

"Nawaamini wachezaji hawa zaidi kuliko wakati wowote ule," alisema Guardiola.

"Sijawahi kuona mchezaji katika maisha yangu anayetamani kufanya vibaya au kutoa uchezaji mbaya kwa mashabiki au kwa klabu. Hakuna anayetaka hivyo.

"Wakati wanapokuwa mbele ya watu 60,000 wanataka kucheza vizuri. Lakini kwa sababu nyingi, inawakwaza."

### MASAIBU YA GUARDIOLA

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona alikuwa na alama kadhaa kwenye paji la uso baada ya mechi hiyo kukamilika alipokuwa akifanya mahojiano na Amazon Prime.

Alipoulizwa na mwandishi kuhusiana na alama yake puani, Guardiola alijibu:" Nilijikwaruza na kucha ya kidole changu."

Baadaye akafanya mzaha kuwa alitaka "kujiumiza" kutokana na timu yake kuwa na matokeo yasiyoridhisha, na kucheka huku akiondoka jukwaani.

Man City hawajakuwa na matokeo mazuri tangu Oktoba 26, mwaka huu, baada ya kufurahia ushindi wa kubahatisha wa bao 1-0 dhidi ya Southampton ambao walikuwa wanasuasua.

Tangu kufungwa mabao 17 katika mechi sita walizozicheza, ni takwimu za kushangaza ukizingatia mafanikio yao chini Guardiola yaliyojikita katika safu imara ya ulinzi.

"Sijui kama ni tatizo la akili," alisema Guardiola.

### KWA NINI SASA?

City ina kibarua kigumu kama inataka kuepuka michezo ya mikondo miwili Februari ili kuingia katika orodha ya timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Itawabidi wamalize katika nafasi ya nane bora ili kupata kibali cha kuingia moja kwa moja katika hatua ya mtoano, lakini wakae nafasi ya 15 baada ya mechi ya Jumanne.

Ingawa wanaweza kushuka hata chini baada ya mechi za Jumatano.

City inasubiri kucheza na timu mbili ambazo zina safu nzuri kama vile Juventus itakayopogwa Jumatano wiki hii na Paris St-Germain Januari 22 kabla ya kuwaalika Brugge Januari 29, mwakani.

"Kwa sasa siko tayari kufikiria kuhusu hayo," alisema Guardiola.

"Tunapaswa kujiandaa vema kwa mchuano ujao. Iwapo tutashindwa kushinda michuano itakuwa vigumu kwetu."

Hata hivyo, Man City wanajitahidi kukabiliana na kumkosa Rodri, kiungo bora wa ulinzi duniani na mshindi wa Ballon d'Or.

## ISIKUPITE

USHINDI wa mabao 3-0 Nottingham Forest iliyoupata dhidi ya Manchester United pale Old Trafford juzi ni wa kwanza kwao katika kipindi cha miaka 30, pia unaifanya United kubaki na pointi zao 19 katika mechi 15, ambazo ndizo chache zaidi kwa klabu hiyo kuzivuna kwa msimu katika hatua kama hii tangu msimu wa 1986-87. Lakini pia Kocha Ruben Amorim ameshinda mechi moja tu kati ya nne za ligi tangu akabidhiwe kijiti cha ukocha mkuu huku kikosi chake kikisalia nafasi ya 13.



## Extra Time




# WANASOKA MASHABIKI WA MPIRA WA KIKAPU NA WAKALI WA MAVAZI

**LONDON, England**

WAKATI michezo miwili mikubwa zaidi duniani inapogongana; soka na mpira wa kikapu, kuna kuwa na mitindo ya kuvutia ya mavazi yakioneshwa, iwe nje ya uwanja au ndani.

Nyota wa Manchester United, Marcus Rashford alizua tafrani kwenye mitandao ya kijamii Novemba aliposafiri kwa ndege binafsi hadi Maddison Square Garden nchini Marekani kuishangilia timu ya New York Knicks ikicheza na Brooklyn Nets kwenye Ligi ya NBA.

Aliwasili akiwa amevalia koti la kifahari la Louis Vuitton kabla ya kukaa kwenye viti ili kuishuhudia timu ya Knicks ikitawala kwa ushindi dhidi ya wapinzani wao.

Ingawa wengine hawakukubaliana na chaguo la Rashford la mapumziko ya mechi za kimataifa, mapenzi yake ya wazi ya mpira wa kikapu yanamfanya ajiunge na orodha ndefu ya wachezaji wa mpira wa miguu ambao ni mashabiki wakubwa wa mchezo huo.

Vinicius Junior, Jude Bellingham na Neymar ni miongoni mwa baadhi ya mashabiki wanaovaa kimaridadi zaidi wakiwa uwanjani kushangilia mpira wa kikapu.

### 5. JUDE BELLINGHAM

Jude Bellingham kwa sasa amefikia kwenye ubora wake na ukamwezesha kujiunga na Real Madrid msimu wa majira ya joto wa 2023.

Ukiachana na kujiunga kwake kule 'Los Blancos', lakini Bellingham sasa amejiimarisha kama shabiki wa mpira wa kikapu.

Na bila shaka, fursa ya kuhudhuria mojawapo ya michezo hii pia inampa mchezaji huyo wa Kimataifa wa England nafasi ya kuonesha baadhi ya mavazi yake bora na kuvutia.

Alionekana akiwa amevalia sweta la bluu la hoodie na jinsi nyeusi Oktoba akiwa uwanjani Marekani.

Kwa kifupi Bellingham anajua jinsi ya kuvaa na anakwenda sambamba na fasheni.

### 4. AURELIEN TCHOUAMENI

Kiungo wa kati wa Real Madrid, Aurelien Tchouameni ni mmoja wa wanamitindo bora kabisa sawa na wachezaji wenzake wachache.

Nyota huyo wa Ufaransa mara kwa mara amekuwa kwenye kurasa za mitindo akiwa nje ya soka. Hata kule Real Madrid anajulikana kwa ustadi wa kutupia mavazi ya kisasa.

Tchouameni anajulikana kwa mtindo wake wa mavazi ya mitaani, na vazi linalojumuisha shati la Migos na suruali ya tracksuit aina ya Essentials inaonesha ustadi wake binafsi.

Mpira wa kikapu ndio furaha yake kuu kushabikia kuliko hata wa miguu.

### 3. MARCUS RASHFORD

Nyota huyu wa Man Utd alikuwa tayari amepata nafasi yake miongoni mwa wachezaji wanaovalia vizuri zaidi kwenye soka, lakini kwa hakika amejiimarisha baada ya kusogea hadi Maddison Square Garden akiwa amevalia vazi la mbunifu Louis Vuitton.

Chini ya nguo zake za kifahari, Rashford alivalia koti, akiunganisha cheni za rangi ya fedha. Pete za Chrome Hearts zilimalizia mtindo huu bora wa kuvutia macho ya mashabiki kila mahali.

Baadaye alifanikiwa kuchukua jezi ya Knicks kutoka kwa mchezaji wa kikapu, Jalen Brunson.

### 2. VINCIUS JUNIOR

Iwe Ligi ya Ulaya au NBA, Vinicius Junior karibu kila wakati utamkuta amekaa siti za mbele kwenye baadhi ya mechi za kusisimua zaidi za mpira wa kikapu.

Vinicius, ambaye inajulikana kuwa ni shabiki mkubwa wa LeBron James, hata alibadilishana jezi na nguli huyo wa Los Angeles Lakers Krismasi iliyopita.

Kwa kawaida, nyota huyo wa Real Madrid kila mara hujitokeza kwa mavazi ya mtindo wa aina yake.

Chapa za hadhi ya juu, cheni kubwa ni miongoni mwa staili anazozipenda Vinicius.

Kwa hakika Vinicius angekuwa nyota wa NBA katika maisha mengine kama si mpira wa miguu.

### 1. NEYMAR

Neymar si tu shabiki mkubwa wa mpira wa kikapu, lakini pia ni mzuri katika kucheza, kwa mujibu wa nyota wa NBA All-Star mara sita, Jimmy Butler.

Unaweza kuchukua neno lake kwa hilo, lakini kilichodhahiri ni mtindo wazi wa mavazi kwa Mbrazili huyo ambao mara nyingi huoneshwa akiwa jukwaani.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona amehudhuria mechi nyingi zaidi za NBA kwa timu ya Los Angeles Lakers.

Na hata timu hiyo humtaja Neymar kama mmoja wa mashabiki wake muhimu.

Mavazi yake daima ni pamoja na cheni nyingi shingoni na mikononi na pete nyembamba vidoleni.

## Nukuu

"Tunataka kuwa wafalme wa kila kitu. Kwa mipira ya kutengwa katika sehemu zilizopangwa, bora zaidi duniani, kwa kushambulia kwa kasi, bora zaidi duniani, kushambulia maeneo ya wazi, bora zaidi duniani. Tunataka mashabiki bora zaidi uwanjani, na kuwa bora katika kila kitu." **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, aliwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wao wa jana, Jumapili dhidi ya Fulham.**



"Nataka kushinda, lakini nataka kushinda kwa usafi na haki. Ikiwa siwezi kushinda kwa uwazi, napendelea kushindwa," **Jose Mourinho akishusha kijembe kwa Pep Guardiola kwa kurejelea mashtaka 115 ya Ligi Kuu ya England dhidi ya City kwa madai ya kukiuka kanuni za kifedha katika usajili.**



"Nawaamini wachezaji hawa zaidi kuliko wakati wowote ule. Sijawahi kuona mchezaji katika maisha yangu anayetamani kufanya vibaya au kutoa uchezaji mbaya kwa mashabiki au kwa klabu. Hakuna anayetaka hivyo, wanapokuwa mbele ya watu 60,000 wanataka kucheza vizuri. Lakini kwa sababu nyingi, inawakwaza," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**



Nipashe
Spotika

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 9, 2024

# REKODI, TAKWIMU HADI RAUNDI YA 13 LIGI KUU KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara iko kwenye mapumziko ya muda mfupi kupisha mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, ambayo hapa nchini inawakilishwa na Simba na Yanga.

Kwa mujibu wa Ratiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), inaonesha itaendelea tena keshokutwa, Jumatano, wakati JKT Tanzania itakapokuwa nyumbani, Meja Jenerali Isamuhyo ikicheza dhidi ya Pamba Jiji na kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, wenyeji Kagera Sugar wataikaribisha Namungo FC.

Mpaka sasa timu nyingi zimefikisha raundi ya 13, lakini baadhi zimecheza mechi 12, na timu chache 11.

Rekodi na takwimu zimeendelea kuwekwa hadi kufikia raundi hiyo, ambazo Nipashe linakuletea katika makala haya na kuwekwa kwenye mtindo wa namba, twende sasa...

**195#** Hii ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia leo hii.

**162#** Ni idadi ya mabao yaliyofungwa na wachezaji kwenye Ligi Kuu wakiwa ndani ya eneo la hatari la wapinzani wao.

**116#** Hii ni namba ya jumla ya wachezaji wote waliofunga mabao yote 195 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi sasa.

**114#** Jumla ya mabao yaliyofungwa kwa mguu wa kulia mpaka sasa hadi kufikia raundi ya 13.

**99#** Ni idadi ya mechi zilizochezwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, baadhi ya timu zikicheza mechi 13, zingine bado zikiwa na michezo 12.

**74#** Hii ni idadi ya mechi za ushindi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Timu zote 16 zilizoshinda, idadi ya mechi zao ukizijulisha unapata namba hii.

**51#** Namba hii inasimama kuwa idadi ya mabao yaliyofungwa kwa mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**45#** Hii ni idadi ya jumla ya mechi ambazo timu zimepata ushindi zikicheza kwenye uwanja wao wa nyumbani.

**33#** Ni jumla ya mabao yaliyofungwa na wachezaji kwenye Ligi Kuu Tanzania bara wakiwa nje ya boksi la hatari.

**31#** Jumla ya idadi ya penalti zilizotolewa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi sasa.

**30#** Ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwa vichwa na wachezaji mbalimbali kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Namba hii inasimama pia kuwa ni idadi ya pointi za Azam FC, inayoongoza ligi.

**29#** Namba hii inasimama kama idadi ya jumla ya mechi ambazo timu imezipata zikicheza kwenye viwanja vya ugenini.

**25#** Hii ni idadi ya jumla ya mechi za sare zilizopatikana mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Pia inasimama kama ni idadi ya penalti zilizofungwa hadi sasa kwenye ligi hiyo.

**22#** Simba imefunga idadi hii ya mabao kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ikiwa ndiyo timu inayoongoza kupachika mabao mengi mpaka sasa.

**20#** Ni idadi ya mabao ya kufunga ya Fountain Gate, ikiwa inashika nafasi ya pili kwa kupachika mabao mengi mpaka sasa, nyuma ya Simba.

**19#** Ni mabao ya kufunga ya Azam FC, ambayo inakamata nafasi ya tatu kwa kufunga mabao mengi mpaka sasa.

**16#** Ni idadi ya mabao ambayo timu tatu za Yanga, Tabora United na Singida Black Stars zimefunga mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, zikiwa kwenye nafasi ya nne kwa kufunga mabao mengi mpaka sasa.

**12#** Namba hii inasimama kama idadi ya mabao ya kufunga ya Coastal Union, lakini pia imefungwa mabao idadi kama hiyo, hivyo tofauti kuwa sifuri.

**11#** Timu tatu ambazo ni Simba, Yanga na JKT Tanzania ambazo zimecheza idadi hii ya michezo kwenye ligi, zikiwa zimecheza mechi chache zaidi kuliko timu zingine.

**9#** KenGold inayoshika mkia ikiwa kwenye nafasi ya 16 na Namungo ambayo ipo nafasi ya 15, ndizo timu zilizopoteza michezo mingi kwenye Ligi Kuu, zikiwa zimepoteza idadi hiyo.

**6#** Ni idadi ya penalti zilizokoswa mpaka sasa, nne zikiokolewa na makipa na mbili wachezaji wenyewe wakipiga nje.

**4#** Namba hii inasimama kama mabao ya kujifunga katika mechi 99 za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizochezwa mpaka sasa.

**1#** Namna hii inaonesha idadi ya mechi ambazo Simba na Azam zimepoteza mpaka sasa kwenye ligi, zikiwa ndiyo timu zilizopoteza mara chache zaidi.

**0#** Hii inasimama kwa timu za Yanga na Namungo kuwa ndiyo timu pekee mpaka sasa kwenye Ligi Kuu ambazo hazijatoka sare yoyote. Yanga imecheza mechi 11, ikishinda tisa na kupoteza miwili, Namungo ikicheza michezo 12, ikishinda mitatu na kupoteza tisa.



Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum maarufu 'Fei Toto', akishangilia bao alilofunga katika mchezo dhidi ya Dodoma Jiji, kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, ikiwa ni moja ya michezo ya mwisho kabla ligi kusimama. Lilikuwa bao la pili kwenye mchezo huo ambao ulimalizika kwa dakika 90, wageni wakishinda 3-1 na sasa wako kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu wakiwa na pointi 30 kwa michezo 13 waliyocheza. **MPIGAPICHA WETU**

## JE, WAJUA?




MANCHESTER City ndio mabingwa wa kwanza wa Ligi Kuu England kupoteza michezo mitano mfululizo katika mashindano yote tangu Chelsea ilipopitia hali hiyo Machi 1956.



## Wenye ulemavu watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WATU wenye ulemavu wamehamasishwa kuunda vikundi vya ujasirimali, ili kuchangamkia fursa za kiuchumi zilizopo ikiwa mikopo ya asilimia mbili inayotolewa kupitia halmashauri.

Pia wametakiwa kushiriki kikamilifu katika masuala ya kisiasa katika uchaguzi ujao kwa kujitokeza kugombea nafasi ya ubunge na udiwani kama walivyojitokeza kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji uliofanyika mwaka huu.

Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Mkoa wa Dodoma (SHIVYAWATA), Justus Ng'wantalima alito rai hiyo kwenye kongamano la maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu iliyofanyika wilayani Bahi.

Ng'wantalima alisema ili wajikwamue kiuchumi watu wenye ulemavu wanapaswa kuchangamkia fursa zilizotolewa na serikali kwenye maeneo yao.

Kuhusu uchaguzi, aliwataka wajiamini na kujidhamini kama walivyojitokeza kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hivyo hivyo washiriki kugombea kwenye nafasi za ubunge na udiwani.

Alisema kuwa wakishiriki kwenye uchaguzi huo watapata nafasi za uwakilishi kwenye vyombo vya maamuzi kuanzia kwenye ngazi ya vijiji, mitaa hadi halmashauri za wilaya na upatikanaji wa mahitaji yao kuwa rahisi kupitia mipango na bajeti.

Mmoja wa wadau wa maendeleo, Eva Mpagama akizungumza kwenye kongamano hilo aliwaomba wadau wenye vipato kuwaangalia kwa ukaribu watu wenye ulemavu kutokana na kero nyingi wanazokabiliana nazo.

Alisema bado makundi hayo wanahitaji kusaidiwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya afya, elimu, chakula, mavazi na malazi huku akidai kuwa maeneo mengi bado hayana miundombinu rafiki.

Vyama vilivyoshiriki kwenye kongamano hilo ni pamoja na Chama cha Viziwi (CHAVITA ) Chama cha Walemavu wa Akili (TAMH), Chama cha Watu wenye Ualbino (TAS) Chama cha Walemavu wa Viungo (CHAWATA).

# Wadau wakoshwa mkakati kuwakinga wenye ualbino

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imepongezwa kwa kuzindua mpango kazi wa kitaifa wa hati na ustawi kwa watu wenye ualbino, kutakiwa kusimamiwa vizuri ili kukomesha mauaji ya watu hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi inayojihusisha na kusaidia watu wenye ulemavu mkoani hapa ya FDH, Maiko Salali, alitoa pongezi hizo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mpango huo.

"Ni imani yetu kuwa baada ya kuzinduliwa kwa mpango huu, tutakwenda kutatua changamoto nyingi zilizokuwa zikiwakabili watu wenye ualbino nchini na kulifanya kundi hili kulifurahia taifa lao sawa na watu wengine walioko katika taifa hili," alisema Salali.

**Na kupunguza matukio mengine ya kikatili ikiwamo wenye ualbino kukatwa viungo vyao kama ambavyo imekuwa ikiripotiwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kutokana na imani potofu za kishirikina.**

Aidha, alisema watu wenye ualbino nchini kwa muda mrefu wamekuwa wakikabiliwa na kero mbalimbali kama vile mitazamo hasi kwa jamii.

Alisema mitazamo hiyo potofu imewasababisha kupata madhira ikiwamo kuuawa, kukatwa viungo na aina nyingine nyingi za ukatili.

"Hivyo ni matarajio yetu watu wenye ualbino nchini kuwa kama mpango kazi huu wa kitaifa wa haki na ustawi kwa watu wenye ualbino nchini utasimamiwa vizuri na serikali kwa kushirikiana na wadau wengine tutafanikisha kukomesha mauaji ya kundi hilo." Alisema na kuongeza:

"Na kupunguza matukio mengine ya kikatili ikiwamo wenye ualbino kukatwa viungo vyao kama ambavyo imekuwa ikiripotiwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kutokana na imani potofu za kishirikina," alisema Salali.

Aidha, alimpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete kwa kuongoza vema mchakato wote wa kufanikisha mpango huo kupitia kitengo cha watu wenye ulemavu kilichoko chini ya ofisi yake.

Alisema FDH inakishukuru Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS), Standing Voice, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) na wadau wengine waliojitolea kuweka nguvu, rasilimali fedha na mchango wao wa kimawazo ambao umefanikisha mpango kazi huo.

Mpango kazi wa kitaifa wa haki na ustawi kwa watu wenye ualbino ulizinduliwa Desemba 3, 2024 jijini Dar es Saalam ikiwa ni sehemu ya utekelezaji maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa bungeni baada ya mauaji ya mtoto mwenye ualbino katika Kijiji cha Bulamula wilayani Muleba mkoani Kagera, Asimwe Novath (2).



Katibu Tawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Sarah Ngalingasi (wa tatu kulia), akimsaidia kumvalisha magongo Mwanaidi Issa, mkazi wa Kondoa baada ya kukabidhiwa kwenye maadhimisho ya watu wenye ulemavu yaliyofanyika kimkoa wilayani Bahi jana. Kutoka kulia ni Katibu wa Shivyawata Dodoma, Jastast Ng'wantalima, Mwenyekiti Omary Lubuva na (kushoto) ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Zaina Mlawa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Asilimia 80 wanafunzi UDOM wanasomeshwa na serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASILIMIA 80 ya wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wanafadhiliwa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye mahafali ya 15 ya chuo hicho.

"Takribani asilimia 80 ya wanaosoma UDOM wanafadhiliwa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kama ingetokea wanafunzi hawa hawajapata ufadhili idadi ya wanafunzi wanaohitimu chuoni hapa ingekuwa ndogo sana," alisema.

Aidha, alisema hivi sasa UDOM imeanza kuvutia wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali ikiwamo Pakstan ambapo kwa sasa kuna mwanafunzi mmoja.

"Naomba niwatoe hofu kuwa elimu tunayoitoa UDOM ni ya viwango na wanafunzi wanaohitimu ambao wamepikwa na kuiva vizuri. Niwapongeze wakufunzi ambao mmekuwa mkisimamia misingi bora ya elimu kwa wanafunzi na kuhakikisha wanamaliza wakiwa na nidhamu," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, Prof. Rwekaza Mukandala, alisema baraza hilo limeendelea kuisimamia mikakati na sera ili kuhakikisha taaluma ya chuo inaendelea kukua.

"Nawapongeza wahitimu waliomaliza masomo yao UDOM. Naipongeza serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya chuo," alisema.

Mmoja wa wahitimu wa Shahada ya Ualimu, Daud Mapelele aliipongeza serikali kwa namna ambavyo imeweka mazingira wezeshi kwa wahitimu kujiajiri pindi wanapohitimu elimu ya chuo ili kuepuka utegemezi.

Alisema (yeye) baada ya kumaliza elimu ya chuo kikuu alijiunga na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) na kupata elimu ya ufundi umeme na kwa sasa amejiajiri na kuajiri wenzake wanne na wote wanapata kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku.





# Wazazi kulala na watoto chanzo ongezeko matukio ubakaji, ulawiti

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa tabia ya baadhi ya wazazi na walezi kulala chumba kimoja na watoto wao, wanawake kuwa kwenye uhusiano na mwanaume zaidi ya mmoja imetajwa kuwa ni chanzo cha kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti.

**Baadhi ya wazazi pia wamekosa ustaarabu ambapo kwa wakati mwingine wanatumia lugha za matusi mbele ya watoto.**

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na baadhi ya wazazi wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Magegele iliyopo Kata ya Kivavi Halmashauri ya Mji wa Makambako wakati wa mkutano wa kupokea taarifa ya shule hiyo.

Walisema mmomonyoko wa maadili unaongezeka kutokana na watoto kujifunza tabia mbaya kutoka kwa wazazi, kwa sababu wengi wao wanalala na watoto hao chumba kimoja hali inayopelekea washuhudie matukio yote wanayoyafanya.

Baadhi ya wazazi hao akiwamo, Daines Sigala alisema kutengana kwa wanandoa na baadhi ya wanawake kuishi na mwanaume zaidi ya mmoja ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili kwa watoto, kwamba wengi wao wanajifunza kile kinachofanywa na wazazi wao kwa vitendo kuliko nasaha wanazozipata kwa maneno.

"Inasikitisha sana wazazi wanafanya mambo mbele ya watoto kwa sababu unakuta wazazi ni wanandoa wamepanga chumba kimoja wamejikinga kwa kuweka pazia ambalo linaonyesha kwa hiyo watoto wanashtuka na wanaona kila kitu kinachoendelea," alisema Sigala.

Naye Goodluck Nyai alisema baadhi ya wazazi pia wamekosa ustaarabu ambapo kwa wakati mwingine wanatumia lugha za matusi mbele ya watoto.

Mwalimu wa malezi katika Shule ya Msingi Magegele, Helen Nziku aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao hasa katika kipindi cha likizo ili kuwalinda na vitendo vya ukatili.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Magegele, Victor Nyato, aliwataka wanawake kutoficha matukio ya kufanyiwa ukatili na waume zao hasa kulawitiwa kwa kuhofia kuachika kwenye ndoa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Magegele, Amosi Mtawa alitoa rai kwa wazazi kuwa kielelezo kwa kutimiza wajibu wao wa kimalezi, ili kuwalinda watoto na matukio ya ukatili kwani wakati wa likizo wanafunzi wengi hupata ujauzito.

Ofisa Elimu Kata ya Kivavi, Shamsa Kandoro alisema walimu wamewakabidhi watoto kwenda likizo wakiwa salama, hivyo ni wajibu wa wazazi kuwalinda watoto hao wasipate adha yoyote ikiwamo ukatili kipindi cha likizo.



Mafundi wakihangaika namna ya kulivusha katapila lisiharibu barabara katika eneo la Kibo Kimara , jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TMDA yaonya matumizi dawa kiholela

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA wa Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani Njombe, wameonywa kutumia dawa pasipo vipimo.

Pia, wameonywa matumizi ya dawa za binadamu kuwapa mifugo.

Onyo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Elimu kwa Umma kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Maria Sanga, wakati akizungumza na wafanyabiashara wa soko kuu na soko la wakulima mjini humo.

Maria alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kuhakikisha wanatumia dawa kwa usahihi kama ambavyo wamepewa maelekezo na wataalamu kwa sababu bila ya kufanya hivyo kunapelekea usugu.

"Kumekuwapo na wimbi la wananchi kutumia dawa pasipo vipimo vya daktari, kutomaliza dawa kwa muda sahihi na wengine kutumia dawa za binadamu kwenye mifugo, niwaombe mkipata changamoto yoyote ya afya na daktari akakwambia tumia dawa hizi kwa muda wa siku kadhaa tumia muda huo huo," alisema Maria.

Maria pia aliwataka vijana na wasichana ambao wamekuwa wakitumia dawa za nguvu za kiume na dawa za kuua mbegu za kiume maarufu (P2) zisitumike kila siku kwa sababu zinaharibu afya zao.

"Watu wamekuwa wakitumia P2 kila wakifanya tendo la ndoa, lakini kitaalamu inatakiwa zitumike mara mbili kwa mwaka na siyo kila wakimaliza tendo la ndoa," alisema.

Aliongeza kuwa: "Kwa wanaume dawa za nguvu za kiume zipo kwa wale ambao wanachangamoto za maumbile yao ya mfumo wa uzazi na siyo kwa watu mbao wazima, mnajiua wenyewe vijana acheni kuwakomoa mabinti mkiamini dawa za nguvu za kiume zinawaridhisha wanawake, hapana."

Naye Mkaguzi wa dawa kutoka TMDA Kanda ya Nyada za Juu Kusini, Adam Sorota aliwataka wananchi ambao watakutana na matatizo yoyote watoe taarifa katika kituo husika walichopata dawa.

Baadhi ya wafanyabiashara mjini Njombe, akiwamo Steward Muhiche alisema ili kuepuka usugu wa dawa elimu inapaswa kutolewa kwa jamii kwa sababu watu wengi bado wanatumia dawa kiholela bila ya kuwaona wataalamu wa afya.

# Madaktari wa Samia watibu wagonjwa 1,756 Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAGONJWA 1, 756 wamepatiwa matibabu katika kambi ya madaktari bingwa na bobezi waliohudumu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe (RRH), kati yao 94 wakifanyiwa upasuaji.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe, Dk. Gilbert Kwesi wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini humo, juu ya tathmini ya kambi ya madaktari bingwa wa Samia wapatao 32.

Alisema kambi hiyo imesaidia kusogeza huduma karibu kwa wananchi ambao ingewalazimu kwenda maeneo mbalimbali ya nchi.

"Huduma hii imetolewa mkoani hapa kwa siku tano, na kambi hii imekuwa na matokeo chanya ya kusaidia wananchi kipindi chote ambacho imefanya kazi hapa," alisema Dk. Kwesi.

Alisema zoezi hilo lilihusisha madaktari bingwa bobezi katika nyanja mbalimbali za afya ikiwamo upasuaji wa aina mbalimbali na magonjwa ya ndani, ambapo wananchi wa mkoa huo wamenufaika na huduma hizo.

"Wagonjwa 14 walipatiwa rufani kutokana na changamoto zao kuwa kubwa zaidi, hivyo kuhitaji kupelekwa katika Hospitali ya Kanda na wachache katika Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisema Dk. Kwesi.

Dk. Kwesi aliyataja magojwa ambayo yalionekana kwa kiasi kikubwa kuwa ni magonjwa ya ndani yanayohusisha mfumo figo na moyo na kufuatiwa na wagonjwa wenye changamoto ya mifupa na maungio.

## MTWARA NA MIAKA 63 YA UHURU...

# RC asimulia mapinduzi yalikofika, ya zamani yamebaki kuwa historia

- Ufaulu juu sekondari 99%; utitiri viwanda
- Malighafi zote Kusini zapitia bandari yao



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala. **PICHA: MTANDAO**

***LEO inaposherehekewa miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania, kuna mengi mazuri yamesimuliwa na kuandikwa kihistoria. Pia, takwimu nyingi zimetolewa kuashiria mema na hatua kubwa zilizopigwa; ya kuvutia na kujivunia.***

***Ndani yake, mikoa ya Kusini Mtwara na Lindi, wakati fulani ikatajwa kukwama kimaendeleo, ikiwamo hali ngumu ya barabara kuu kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara, pia Tunduru, Ruvuma. Je, leo ikoje katika miaka 63 ya uhuru wa nchi? Pata ufafanuzi wa mazungumzo ya maswali na majibu, kutoka kwa Mkuu wa Mkoa, Kanali Patrick Sawala. Fuatilia:***

==

**SWALI:** Zama zile mlifikiwa na mchakato wa Vijiji vya Ujamaa na maendeleo yake. Leo hii mkoje na mlichovuna ndani yake?

**MAJIBU:** Hadi sasa vijiji vyote 785 vina umeme. Katika miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara, nchi haikubaki nyuma kuhakikisha wananchi katika maeneo yote vijijini na mijini wanapata huduma ya umeme. Hivyo mwaka 2007, ilianzishwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ambayo ina jukumu la kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya nishati bora vijijini kwa kutoa ruzuku, mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa waendelezaji wa miradi.

Kutokana na kuanzishwa kwa wakala huo, imeshuhudiwa jinsi umeme ulivyoanza kusambaa kwa kasi katika vijiji mbalimbali nchini na kuanza kubadilisha hali ya uchumi ya wananchi kutokana na kuanzisha shughuli mbalimbali za maendeleo zinazotegemea nishati ya umeme.

Ndani ya Miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara mpaka kufikia Oktoba 2024, utekelezaji miradi ya nishati ya umeme vijijini umewezesha vijiji vyote 785 vya mkoa wa Mtwara kupata umeme.

Uunganishaji umeme vijijini umewezesha taasisi za afya, shule, nyumba za ibada na maeneo ya biashara kufikiwa na huduma za umeme, hivyo kuboresha na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma.

**AFYA NA ELIMU**

**SWALI:** Katika eneo la 'roho ya watu' afya, una maoni gani?

**MAJIBU:** Mtu mwenye afya njema huwa na nguvu ya kujitafutia riziki ya halali na kutimiza wajibu wake. Kwa kulifahamu hilo, baada ya Tanzania Bara kupata uhuru wake mnamo 1961, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliunda wizara inayosimamia Sekta ya Afya, ili kupambana na adui maradhi.

Kabla ya uhuru, mkoa wa Mtwara (ambao ulikuwa ndani ya jimbo la Kusini) ulikuwa na vituo vya kutoa huduma saba, ambazo hospitali zilikuwa tatu na zahanati nne zote zilijengwa na kuendeshwa na Wamisionari wa Kijerumani wa Shirika la Benedictine na Wamisionari wa Shirika la Anglican - Universities Mission to Central Africa (UMCA).

Hatua kubwa imepigwa katika Sekta ya Afya, kupambana na adui mkubwa maradhi, kuanzia wakati wa uhuru wa Tanganyika na mpaka sasa nchi inapoadhimisha miaka 63 ya Uhuru.

Huduma za afya nchini zimeendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha. Hii ni kutokana na mabadiliko endelevu yanayofanyika katika Sekta ya Afya, kwa lengo la kuleta uwiano katika upatikanaji huduma bora za afya mijini na vijijini.

Kwa Mkoa wa Mtwara, idadi ya vituo vya kutoa huduma za afya, imeendelea kuongezeka na hadi kufikia Oktoba, una jumla ya vituo 334. Kati ya hivyo, hospitali ni 11 ikiwamo Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini, vituo vya afya 49 na zahanati 274.

**SWALI:** Maendeleo ya afya, huendana na elimu. Fafanua nafasi ya watu wa Mtwara?

**MAJIBU**: Sekta ya Elimu ni moja ya eneo tumeshuhudia mabadiliko makubwa nchini, ikiwa ni juhudi za kumkomboa Mtanzania kutoka katika ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumwongezea ujuzi na maarifa.

Mabadiliko hayo pia yanaonekana katika mazingira ya kujifunzia na kufundishia, serikali imekarabati, imejenga na kununua vifaa vya kutosha vinavyoendana na mabadiliko ya teknolojia na kuboresha maslahi ya kazi na taaluma ya ualimu, usimamizi wa elimu na mageuzi makubwa katika sayansi, teknolojia na ubunifu na usimamizi wa elimu.

Mkoa wa Mtwara kwa miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania bara, unajivunia mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu, ambayo mpaka sasa kuna jumla ya shule 718 za awali, 702 zikiwa ni za serikali na 16 binafsi.

Kuna shule za msingi 717, huku 702 zikiwa ni za serikali na 15 binafsi, shule za sekondari 193, zikiwamo 179 za serikali na 14 binafsi.

Kwa upande wa elimu ya chuo, mkoa wa Mtwara una vyuo vikuu vitatu, viwili vya serikali na kimoja binafsi.

Mafunzo ya elimu ya ualimu kabla ya uhuru yalikuwa yakitolewa na mashirika ya dini, lakini kwa sasa mkoa wa Mtwara una vyuo vitatu vya ualimu, vyote ni vya serikali.

Aidha, mkoa una vyuo vitatu vya mafunzo ya ufundi stadi (VETA) vyote vikiwa ni vya serikali, pia una vyuo vitatu vya maendeleo ya wananchi (FDCs) ambavyo vinamilikiwa na serikali.

Tanganyika ilipopata Uhuru mwaka 1961, ilirithi utumishi wa umma, ambao jukumu lake kubwa lilikuwa kuhudumia na kulinda masilahi ya serikali ya kikoloni.

Katika kipindi hicho, nchi ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa watumishi wazawa wenye sifa na taaluma mbalimbali za kuwawezesha kutekeleza majukumu ya taasisi mpya zilizoanzishwa.

Kwa sasa, mkoa wa Mtwara una jumla ya walimu 7,586 wa shule za msingi na sekondari, kati ya hao 868 ni walimu wa sayansi na hisabati kwa shule za sekondari.

Mikoa ya Kusini ikiwamo Mtwara, haikuwa na historia nzuri katika suala la elimu, lakini tunapoadhimisha Miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania, mafanikio yanayofikiwa katika elimu kwa mkoa wa Mtwara ni jambo la kujivunia, kwani ufaulu wa wanafunzi wanaofanya mitihani ya kitaifa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

**SWALI:** Unaweza kutoa mfano kuthibitisha?

**MAJIBU:** Ndiyo! Mfano, ufaulu wa wanafunzi wanaopata daraja kwanza hadi la tatu katika kidato cha sita umefikia asilimia 99.9.

Mwaka 2023, ni mwanafunzi mmoja tu aliyepata Daraja la Nne. Ufaulu kwa kidato cha nne umeongezeka kufikia asilimia 92.28 mwaka 2023 huku mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ufaulu umeongezeka kufikia asilimia 79.07 mwaka 2023.

**SWALI:** Hali ya teknolojia ikoje?

**JIBU:** Kabla ya Uhuru, teknolojia ya habari na mawasiliano iliyokuwa inatumika, ilikuwa ya analojia na baadaye tuliingia kwenye mfumo wa digitali. Mkoa wa Mtwara ulikuwa na kituo kimoja cha televisheni kilichomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Baada ya Uhuru, mkoa wa Mtwara uliendelea kuwa katika nyanja ya mawasiliano kupitia Radio Tanzania (RTD) na baadaye Shirika la Utangazaji la Tanganyika (TBC).

Mpaka sasa mkoa wa Mtwara una jumla ya vituo saba. Hadi mwaka 1995 huduma za simu kwa mkoa wa Mtwara zilikuwa zikitolewa na kampuni ya TTCL tu. Kwa sasa kampuni sita za simu zinatoa huduma zake katika mkoa huu.

Mafanikio mengine katika sekta ya teknolojia ndani ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara ni mkoa kuunganishwa na ulimwengu wa intaneti kupitia Makondenet na kampuni ya simu ya TTCL na sasa upo Mkongo wa Taifa, kwa ajili ya kuboresha mawasiliano.

**SWALI:** Tuhamie ilikofika na ilikotoka Mtwara na uchumi, pia miundombinu?

**JIBU:** Uendelezaji miundombinu mbalimbali, zikiwamo barabara, reli, madaraja, viwanja vya ndege na bandari ni sehemu muhimu katika ukuaji wa uchumi na hasa biashara za ndani na nje ya nchi. Mkoa wa Mtwara una miundombinu mizuri ya ardhini, majini na angani ambayo ni kiunganishi muhimu cha mikoa na nchi jirani.

Kwa sasa mtandao wa barabara una jumla ya kilometa 7,446.79. Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA) mkoa wa Mtwara unahudumia jumla ya barabara zenye urefu wa kilomita 6,133.79 zikijumuisha barabara za lami na za changarawe.

Wakala wa Barabara (TANROADS) yenyewe inahudumia barabara yenye urefu wa kilomita 1,313 zikiwamo barabara kuu za lami na za changarawe.

Kuimarisha utengamano wa kibiashara katika ukanda wa kusini, kwa lengo la kupunguza umaskini na kuboresha kiwango cha maisha ya wananchi, mkoa wa Mtwara kupitia TANROADS unajenga barabara ya lami ijulikanayo kama 'Mtwara corridor' itakayounganisha wilaya zake zote tano (Mtwara, Tandahimba, Newala, Masasi na Nanyumbu) pamoja na mikoa na nchi jirani.

Ujenzi wa barabara unaenda sambamba na kuhakikisha kuwa ukarabati wa barabara hizo unafanyika mara kwa mara, hii ikiwa ni pamoja na barabara ambazo bado hazijakamilika kwa kiwango cha lami, zinakuwa katika hali nzuri, uwekaji wa taa za barabarani.

Aidha, ujenzi wa madaraja kwenye barabara hizo unaendelea, ili

INAENDELEA UK. 19



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, akiongea jambo na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Rais mstaafu Jakaya Kikwete baada ya kishiriki mbio za UDSM Marathon 2024 zilizofanyika juzi Kampasi ya Mlimani kwa lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi chuoni huko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mama anusurika kuuawa kwa panga na mwanawe

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

MKAZI wa Kitongoji cha Gudugudu, Kata ya Mlali wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro, Unnu Martin (70), amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, baada ya kunusurika kuuawa kwa kukatwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake na mtoto wake wa kiume.

Kwa mujibu wa taarifa zilizothibitishwa na wanafamilia wa kijana huyo, tukio hilo lilitokea Desemba 6 mwaka huu saa nne asubuhi baada ya mtuhumiwa aliyejaribu kufanya mauaji, Elias Paulo (38) kutoroka hospitalini alikokuwa amepelekwa akisumbuliwa na changamoto ya ugonjwa wa akili.

Mke wa mtuhumiwa huyo, Evarista Matei alisema mumewe anakabiliwa na changamoto ya ugonjwa wa akili kwa muda mrefu, ingawa tatizo hilo lilitulia hadi lilipojitokeza usiku wa kuamkia siku ya tukio la shambulizi kwa mzazi wake.

„Alikuwa hospitalini, lakini ghafla tulishangaa amerudi nyumbani na kuchukua panga na kumvamia mama yake mzazi na kuanza kumkatakata sehemu mbalimbali za mwili wake kama mnavyoona, ikiwamo kichwani, mkononi na kwenye mguu hadi akapoteza fahamu," alidai Evarista.

Alidai kuwa alipoona hali hiyo alipiga kelele kutafuta msaada wa majirani ambao wengi walikuwa mashambani na walipofika walisaidiana kumchukua mama wa kijana huyo na kumkimbiza kituo cha afya jirani kwa matibabu zaidi kabla ya kuhamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Alidai kuwa usiku wa kuamkia siku ya tukio, mumewe alikuwa akiongea mambo yasiyoeleweka yaliyomtisha na kulipokucha alimwomba kwenda naye hospitalini, lakini licha ya kukubali, akiwa huko, aligoma kuchomwa sindano na baadaye akatoroka.

Kaka wa mtuhumiwa huyo, Paulo Paulo alidai ndugu yake kwa kipindi cha nyuma alishawahi kukabiliwa na changamoto ya ugonjwa wa akili. Alidai chanzo cha ugonjwa huo ni matumizi ya dawa za kulevya.

„Matatizo haya ya ugonjwa wa akili yalichangiwa na uvutaji wa bangi, na alipatiwa matibabu kwa karibu miaka saba iliyopita na kuacha kabisa uvutaji, lakini kwa tukio hili nina wasiwasi huenda alirudia tena kuvuta, maana hata majirani wanasema alikuwa anavuta ingawa kila nikimwuliza alikuwa anakataa," alidai Paulo.

Alidai kuwa baada ya kumshambulia mama yao, mtuhumiwa huyo alikimbia na baadaye kurudi tena nyumbani na kuanza kufukia damu ya mama yao iliyosababishwa na kujeruhiwa.

Ofisa Muuguzi na Msimamizi Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Frank Kalinga alithibitisha hospitali hiyo kumpokea majeruhi huyo mwanamke na anaendelea kupatiwa matibabu.

„Mwanamke huyu amepokewa majira ya saa tisa mchana, akitokea Kituo cha Afya Mlali alikokuwa tayari amepatiwa huduma ya kwanza na alikuwa na majeraha matatu kichwani, mawili mkono wake wa kulia na lingine kwenye mguu wa kulia na mengi ya majeraha yalikuwa yalivuja damu ila kwa sasa anaendelea vizuri baada ya matibabu," alisema Kalinga.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Gudugudu, kata ya Mlali, Iddi Hassan, alisema alipokea taarifa za tukio hilo majira ya saa nne asubuhi na alikwenda eneo la tukio ambapo alimkuta mama huyo akiwa amefichwa nyuma ya nyumba huku damu ikimwagika.

Alidai kijana aliyefanya uvamizi huo na kujeruhi alikuwa na changamoto ya ugonjwa wa akili na miaka ya nyuma, hata kijana huyo aliwahi kushambuliwa kijiji jirani na wananchi na kujeruhiwa kwa mapanga akiwa amerukwa na akili na kufanya matendo ambayo yalifanya wanajamii wasiomfahamu kudhani ni mwizi.

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE

Kituo cha JUMUISHO Mkoa DAR ES SALAAM

Usimamizi wa Mirathi Na. 1859 / 2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU NURSALI MOHAMEDI ISERE WA MACHINJIONI

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA

NA

SUDY MURSALY ISSERE

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwazo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 18 Mwezi 11 Mwaka 2024**

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **SHAIBU SIRAJU HASHIMU** amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 400 CRM** aina ya **TOYOTA LITEACE NOAH** chassis namba **SR400218046,** engine **3S412806F.** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/46848/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **EBENEZER JOURNEYS** LIMITED amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 643 EBU** aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** colour **BEIGE** chassis namba **JTERB71J300034494,** engine **1HZ0522025.** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/46850/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISAWAFO GABRIEL AKYOO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 400 CRM – TOYOTA LITEACE NOAH** lenye jina la umiliki wa **SHAIBU SIRAJU HASHIMU.** CHASSIS NUMBER: **SR400218046.** ENGINE NUMBER: **3S412806F.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/46848/2024.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MTWARA

KITUO CHA MIKINDANI MKOA MTWARA

SHAURI LA MADAI/NDOA NAMBA 183 / 2024

JINA LA MDAI MRASA HERMAN MBOTE

NA

JINA LA MDAIWA ASHURA RASHID

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)

**KWA ASHURA RASHID**
**WA DAR ES SALAAM**

**KWAKUWA MDAI/WADAI AMELETA/WAMELETA MADAI YAKE/YAO KWAMBA MADAI YA PESA TSH. 3,380,000/=**

KWA HIYO unatakiwa kuhudhuria bila kukosa katika Mahakama tarehe 04 Mwezi 12 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa Shaurini mahakama inaweza kutoa hukumu bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 11 mwaka 2024.

HAKIMU

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MTWARA

KITUO CHA MIKINDANI MKOA MTWARA

SHAURI LA MADAI/NDOA NAMBA 183 / 2024

JINA LA MDAI MRASA HERMAN MBOTE

NA

JINA LA MDAIWA SAID JUMA MSANGA

KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)

**KWA SAID JUMA MSANGA**
**WA DAR ES SALAAM**

**KWAKUWA MDAI/WADAI AMELETA/WAMELETA MADAI YAKE/YAO KWAMBA MADAI YA PESA TSH. 3,380,000/=**

**KWA HIYO** unatakiwa kuhudhuria bila kukosa katika Mahakama tarehe 04 Mwezi 12 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa Shaurini mahakama inaweza kutoa hukumu bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 11 mwaka 2024.

HAKIMU

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 27818 OF 2024

In the Matter of the estate of the late of EMMANUEL OBED KITUNDU of Nzuguni within Dodoma City

And

In the matter of an application for Letters of administration by PENDO PAUL KYAMBA

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 17 day of 1...................... 2025

Dated at Dodoma this 6 day of 12......................2024

RESIDENT MAGISTRATE

## MTWARA NA MIAKA 63 YA UHURU...

# RC asimulia mapinduzi yalikofika, ya zamani yamebaki kuwa historia

INATOKA UK. 17

kuweza kuunganisha mawasiliano kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuzifanya barabara hizo ziweze kupitika kwenye majira yote ya mwaka ambapo tayari TANROADS imetenga shilingi milioni 77.25, kwa ajili ya ujenzi wa madaraja 93 katika barabara kuu.

**USAFIRI ANGA, MAJINI**

**SWALI:** Usafiri wa anga ni sehemu ya mtaji wa maendeleo kitaifa. Hapo nakurejea wa Mtwara, mkoje?

**MAJIBU:** Kwa sasa mkoa wa Mtwara una viwanja viwili vya ndege, Mtwara na Masasi. Serikali inaendelea kuimarisha usafiri wa anga, ambayo inafanya maboresho ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mtwara, kwa lengo la kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji, ili kiweze kuhudumia ndege kubwa za ndani na nje ya nchi zenye ukubwa wa Boeing 787-8 (Dreamliner).

Aidha, unafanyika ukarabati na upanuzi wa majengo ya kiwanja ikihusisha ujenzi wa jengo la abiria, kuongozea ndege, kituo cha zimamoto na ujenzi wa jengo la hali ya hewa.

Miradi hii imetekelezwa chini ya usimamizi wa TANROADS kwa gharama ya shilingi bilioni 56.99. Utekelezaji huo umefikia asilimia 98 huku ukitegemewa kuzidi kufungua fursa zaidi za kiuchumi.

**SWALI:** Upande kama huo majini, manajivunia kipi?

**MAJIBU:** Jitihada kubwa zimefanywa na serikali ndani ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara, katika kuhakikisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji inafunguliwa na kuwafikia wananchi, ikiwa ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Mamlaka ya Bandari imefanya upanuzi wa Bandari ya Mtwara, imejenga gati moja jipya lililogharimu shilingi bilioni 157.8. Sasa bandari ina uwezo wa kuhudumia meli zenye ukubwa wa hadi wa GRT 35,607 na urefu wa mita 199.98 ambazo zinabeba shehena ya makaa ya mawe hadi tani 59,960 kwa mara moja.

Pia, ina uwezo kuhudumia shehena milioni moja na laki sita, kutoka laki nne zilizokuwa zikihudumiwa kwa mwaka. Aidha Bandari ya Mtwara, inasafirisha korosho zote zinazozalishwa kwa mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi na Ruvuma).

Bandari ya Mtwara imefanya ununuzi wa boti iliyogharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 1,696,068. Lengo ni kuongeza ufanisi na tija katika kuhudumia meli zinazowasili bandarini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipotembelea kiwanda cha korosho mkoani Mtwara.. **PICHA : MTANDAO**

**KILIMO, HUDUMA MAJI**

**SWALI:** Kihistoria inadumu harakati na kampeni 'Maji ni Uhai'. Enyi wana- Mtwara imewafikiaje?

**MAJIBU:** 'Maji ni Uhai' ni usemi ambao umekuwa ukisikika kwa masikio ya walio wengi. Miaka 63 ya uhuru, mkoa wa Mtwara umeshuhudia miradi mikubwa ya maji inayolenga kuwapatia wananchi maji safi na salama na yenye kutosheleza.

Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuongeza upatikanaji wa maji salama katika makazi ya mijini na vijijini ambapo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara (MTUWASA) inahudumia Manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya mji Nanyamba.

Huku Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi - Nachingwea (MANAWASA), ikihudumia Masasi na Nachingwea kupitia mtandao wa maji unaotoa kwenye vyanzo vya Mbwinji. Mamlaka ya Maji Makonde inahudumia Wilaya za Newala na Tandahimba.

Aidha, Mamlaka ya Maji MTUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Mkoa wa Mtwara, ipo kwenye maandalizi ya mradi mkubwa utakaotoa maji kutoka Mto Ruvuma. Mradi huu utaweza kuhudumia viwanda mbalimbali vinavyotarajiwa kujengwa ndani ya miaka 20 ijayo.

**SWALI:** Tuhamie shambani, kwenye 'Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa'. Mtwara mnachangaje hisa hizo kitaifa?

**MAJIBU:** Kupitia kilimo, Watanzania wanajipatia chakula cha kutosha, hivyo kupunguza tatizo la utapiamlo nchini. Wakati taifa likisherehekea miaka 63 toka limepata Uhuru, Sekta ya Kilimo nayo imekua.

Shughuli zinazohusiana na kilimo zinachukua asilimia 85 ya shughuli za kiuchumi zinazofanyika mkoa wa Mtwara. Mkoa unalima mazao ya chakula yakiwamo muhogo, mpunga, mahindi, ulezi, ndizi, viazi vitamu, mtama, maharage na mikunde.

Mazao makuu ya biashara ni korosho, ufuta na mbaazi, ambayo yanauzwa kwa mfumo wa Stakabadhi Ghalani, kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), ambao umetengeneza mazingira ya ushindani katika ununuzi wa mazao.

Ni hali iliyosababisha wakulima kuwa na uhakika wa bei za mazao wanayozalisha, huku halmashauri katika maeneo husika, pia zikinufaika kupitia kodi kutokana na ongezeko la bei.

Mkoa unajitosheleza kwa chakula huku ukiwa na ziada ya tani 618,425 za zao la muhogo uliozalishwa katika msimu 2022/23.

Katika kuihakikisha kilimo mkoani Mtwara kinakua, Wizara ya Kilimo, Bodi ya Korosho na Tume ya Ushirika, zimetoa jumla ya pikipiki 274 kwa maofisa ugani, maofisa kilimo na maofisa ushirika. Aidha, msimu wa mwaka 2023/2024, kuna jumla ya wakulima 334,565 walisajiliwa kunufaika na ruzuku za pembejeo zinazotolewa na serikali huku tani 4,513 za mbolea za kupandia na kukuzia zikitumika.

Mkoa wa Mtwara kwa msimu wa 2024, umepokea pembejeo za ruzuku ya zao la korosho, salfa ya unga tani 21,382 na viuatilifu vya maji lita 862,075.

Katika msimu wa 2024/25, hadi kufikia tarehe mbili, Desemba 2024, tayari kuna tani 225,396.44 za korosho zenye thamani ya shilingi bilioni 831 zimeuzwa, huku bei ya juu ikishuhudiwa kuwa maradufu ya miaka ya zamani.

Imefikia shilingi 4,195 wakati bei ya chini ikiwa 2,110. Bandari ya Mtwara inatumika kusafirisha korosho zinazokwenda nje ya nchi kutokea mikoa ya Lindi, Ruvuma na Mtwara.

**VIWANDA, BIASHARA, UWEKEZAJI**

**SWALI:** Huduma ya maji na kinachozalishwa shambani, sehemu yake huhitajika kama rasilimali viwandani. Mtwara mnasemaje katika kigezo hicho kingine cha kiuchumi?

**MAJIBU:** Ni dhahiri sekta ya viwanda na biashara, ina mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi shindani, inachochea na kuimarisha ukuaji wa uzalishaji wa ndani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara.

Katika sekta ya viwanda, mkoa una jumla ya viwanda vikubwa 23 vinavyoendelea na uzalishaji, kati ya hivyo viwili ni viwanda vya saruji, 16 viwanda vya kubangua korosho, viwili vya kuchakata gesi, kimoja cha chaki, kimoja cha kuchakata chumvi na kimoja ni kiwanda cha maji ya kunywa. Viwanda hivyo vimetoa ajira zaidi ya 4,731.

Aidha, vipo viwanda vidogo vidogo zaidi ya 130 vilivyotoa ajira 1,680. Viwanda hivi vinavyojishughulisha na uzalishaji bidhaa mbalimbali kama vile sabuni, mafuta, kusindika vyakula, ushonaji, uselemala, kufyatua matofali na zinginezo.

Mkoa wa Mtwara katika kuvutia wawekezaji kwenye Sekta ya Viwanda na kuhakikisha viwanda zaidi vinajengwa umeendelea na jitihada za kutenga na kupima maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo. Pia (mkoa) unatarajia kuanza ujenzi wa Ofisi ya Wajasiriamali na Watoa Huduma Wadogo (Machinga), mradi utakaogharimu zaidi ya shilingi milioni 39.

**SWALI:** Mkuu, kuna lulu nyingine ya uchumi Wizara ya Maliasili na Utalii. Mtwara mmepiga hatua gani?

**MAJIBU:** Ikumbukwe kuwa juhudi za kuhifadhi na kulinda rasilimali za maliasili zilikuwapo hata kabla ya ukoloni, ambayo jamii nyingi nchini zilitenga maeneo maalumu ya misitu kwa ajili ya shughuli za ibada na matambiko.

Mkoa wa Mtwara, una maeneo mazuri yenye vivutio vya utalii. Baadhi ya maeneo ni pamoja na: Shimo la Mungu, Chilolelo na Maporomoko ya Milima ya Makonde (Makonde Escarpment) wilayani Newala. Mlima na Pango la Mkomaindo wilayani Masasi.

Hifadhi ya Wanyamapori ya Lukwika/Lumesule na Msanjesi Wilayani Nanyumbu. Mji wa kihistoria wa Mikindani ambao unatumika kama kituo cha biashara Kusini mwa Tanzania na wenyeji wa mji huu ni wa Makonde. Ndani ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania, Mkoa wa Mtwara bado una ufukwe nzuri ambazo hazijaharibiwa na shughuli za kibinadamu. Katika kuenzi na kutangaza kivutio hicho, mkoa na wadau huadhimisha 'Tamasha la Msangamkuu' kila mwishoni mwa mwaka.

Tamasha hili uhusisha maonesho ya shughuli za uhifadhi na utalii pamoja na michezo mbalimbali ya baharini.

Aidha, Ghuba ya Mnazi 'Mnazi Bay Marine Park' iliyopo katika Kata ya Msimbati, wilaya ya Mtwara imekuwa ikipokea samaki aina ya nyangumi, ambao huja kwa lengo la kuzaliana katika kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba kila mwaka.

Mkoa kwa kushirikiana na wadau wa utalii umetumia fursa hiyo kubuni tamasha lijulikanalo kama 'Nyangumi Festival'.

- ***Kesho usikose simulizi ya mkongwe wa Mtwara na Uhuru wa Tanganyika, marehemu Nangwanda Sijaona.***

# *VETA INAVYOIJENGA TANZANIA HURU*

## Tunapoadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika, hebu kwanza tujikumbushe maono ya Viongozi wetu:



*Dtk Mhe.samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania*



***Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere***
***Rais wa kwanza waJamhuri wa Muungano wa Tanzania***

Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, wakati akihutubia katika Mkutano wa 29 wa Baraza la Kutunga Sheria (yaani Bunge), mwaka 1954, alisema, "Tuna uhitaji mkubwa wa elimu ya ufundi na natumaini utoaji wake utaendelea kupanuka."

Katika maadhimisho ya Miaka 20 ya Sera ya Elimu ya Kujitegemea, tarehe 12 Septemba 1988, Mwalimu Nyerere alisisitiza tena juu ya umuhimu wa elimu na mafunzo hayo katika maendeleo ya nchi. Alisema, *".....kwa hiyo, napenda sasa kusisitiza juu ya elimu ya kisayansi na teknolojia na utoaji mafunzo ya ujuzi. Tija yetu, kama binadamu na kama Taifa lina ugonjwa mbaya sana wa kukosa watu wenye ujuzi na kukosa uelewa juu ya misingi ya kisayansi na uhusiano wake na maisha. Nimeelezwa kuwa zaidi ya vijana 360,000 wanamaliza elimu ya msingi na maelfu elimu ya sekondari bila kuwa na ujuzi mahsusi wa aina yoyote, ambao unaweza kuwasaidia kuanza shughuli za uzalishaji katika jamii baada ya kuhitimu."*

Maono na kipaumbele juu ya mafunzo ya ufundi stadi sasa vinapewa nguvu zaidi na *Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*. Wakati akizindua Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera, tarehe 13 Oktoba, 2022, Mhe. Rais alisema, *"Tunazungumzia tatizo la kutokuwa na ajira, tunasomesha watoto lakini hawana ajira... Kazi yetu ni kuhakikisha tunawajengea uwezo vijana kwa kuwapatia ujuzi ili waweze kuingia kwenye soko la ajira kwa kujiajiri na kuajiriwa,"*



**CPA Anthony Mzee Kasore*Mkurugenzi Mkuu, VETA***

Sisi VETA tunapokumbuka juu ya kauli za viongozi wetu, maono na mikakati yao, tunapata nguvu na hamasa kubwa kuendeleza juhudi za kuijenga nchi yetu kupitia utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa ubora na kwa upana.

*Hatua tulizopiga katika upanuzi wa fursa za mafunzo*

- Tulianza mwaka 1995 tukiwa na vyuo 14 tu, sasa tuna vyuo 80 katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini.
- Tulianza na fani (stadi) 36, sasa ziko 88
- Tulianza na udahili wa wanafunzi 1,940, sasa tumefikia 83,000
- Sekta za Mafunzo zimeongezeka kutoka 10 hadi 13

***Ufikiaji wa makundi mbalimbali***

- Programu ya Mafunzo ya Kukuza Ujasiriamali katika Sekta Isiyo Rasmi (INTEP), tangu kuanza kwake mwaka 2002, imenufaisha zaidi ya wajasiriamali 10,000.
- Mpango wa Kurasimisha ujuzi uliopatikana Nje ya Mfumo Rasmi (RPL) , tangu kuanzishwa kwa mpango huu mwaka 2012 hadi sasa (2024) wanagenzi 23,460 wameshafanyiwa tathmini na kurasimishiwa ujuzi wao.

*Ushirikiano na viwanda katika utoaji Mafunzo*

- Ushirikiano viwanda /waajiri umeendelea kuongezeka na sasa VETA inashirikiana na makampuni zaidi ya 100 katika utoaji mafunzo.
- Programu ya Uanagenzi Pacha (Dual Apprenticeship System-DATS), ambayo imekuwa ikiendeshwa kwa ushirikiano na makampuni mbalimbali, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2011, jumla ya wanagenzi 224 wamehitimu na kuajiriwa huku makampuni 186 yakishiriki kutekeleza mpango huu.
- Programu ya Mafunzo Jumuishi ya Ufundi kwa ajili ya Sekta ya Madini (IMTT) kwa ushirikiano na Chemba ya Madini na Nishati Tanzania (TCME), tangu kuanzishwa kwake mwaka 2008 hadi 2021, jumla ya vijana 1,242 wamenufaika kwa kupatiwa mafunzo kupitia mpango huo ambapo 721 kati yao wamejiajiri na wengine kuajiriwa. Pia kampuni zinazofadhili wanafunzi katika mpango huu zimeongezeka kutoka kampuni mbili za awali hadi kampuni 10 mwaka huu.

***Uendelezaji Ubunifu***

- Jumla ya wabunifu 118 wameibuliwa, 45 wameingizwa kwenye mpango wa uendelezaji na 13 wamebiasharisha ubunifu wao.

***Matokeo yanaonekana***

- Wahitimu wa VETA wanapata ajira kwa urahisi. Utafiti wahitimu wa Ufundi Stadi (Trace Study) uliofanyika mwaka 2023, ukihusisha wahitimu wa miaka mitano kutoka 2017 hadi 2021 ulibaini kuwa asilimia 67.7 ya wahitimu wa ufundi stadi waliajirika, huku waliosalia ama walikuwa wanaendelea na mafunzo ya ngazi za juu au wanafanya kazi za kujitolea.
- Matokeo chanya kiuchumi na kijamii ambayo yanachangiwa na mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vya VETA sasa yanaifanya kuwa kimbilio la wananchi wa makundi mbalimbali.

***Uhuru ni kazi na Kazi inaendelea***

Ujenzi wa vyuo 65 unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini, hadi mwisho wa mwaka 2025, matarajio ni kuwa na vyuo vya VETA 145, ambapo kila wilaya nchini itakuwa na chuo walau kimoja cha ufundi stadi kinachomilikiwa na VETA.

***Ungana nasi***

Jiunge na mafunzo ya ufundi stadi

## TOLEO MAALUM


MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

(VETA)

# MAADHIMISHO YA MIAKA 63 YA UHURU WA UHURU WA TANGANYIKA

9 DESEMBA 2024




VETA Tunaungana na Watanzania wote kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika.

**KAULI MBIU:**

*"UONGOZI MADHUBUTI NA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI NI MSINGI WA MAENDELEO YETU"*

UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA

www.veta.go.tz | 0755 267 489

# Uuzaji kiwanda waliza serikali na wakulima

INATOKA UK.9

cha mpango wa kuwa na nchi ya viwanda.

"Wakulima tunanyanyasika, mashamba mengi yamekufa kwa sababu chai imekosa soko, wakulima wameamua kubadili gia kwa kuikata miche ya chai na kupanda miti ya mbao," analalama Ramadhani.

Kama ilivyo kwa mtangulizi wake Sharifu, Ramadhani anasema kusitishwa uzalishaji kiwandani huko, kumesababisha maisha yao kuwa magumu. Hawana tena fedha za kuwawezesha kujikimu kimaisha huku kukiwa na lingine la ziada -- mzunguko wa fedha katika eneo hilo umekuwa mdogo kulinganishwa na kipindi ambacho kiwanda kilikuwa kinafanya kazi.

"Kiwanda kikifunguliwa uchumi utarejea kama ulivyokuwa awali. Mzunguko wa fedha utakuwa mkubwa kuanzia kwa bodaboda mpaka kwa wachumaji chai. Hivi sasa wapo wanaokata chai kwa kukosa soko, wengine wanasubiri mvua ianze kunyesha ili wapande miti ya mbao katika mashamba ya chai," anasema Ramadhani.

Anasema zaidi ya wakulima 6,000 walikuwa wananufaika na kiwanda hicho kupitia kilimo cha chai. Hao ni kutoka vijiji vya Mtunda, Baga, Kihangala na Dule B ambao Ramadhani anawataja "wamelima mashamba makubwa kutokana na kuwa na uhakika wa soko karibu na mashamba yao." Kiwanda hicho kiko kijijini Mtunda, kata ya Dule B.

Mkulima mwingine wa chai kijijini Mtunda, Anna Shemdoe, anasema, "tunateseka sana kwa sababu hatuna pa kupeleka chai yetu, tunakosa fedha kwa ajili ya kusomesha watoto. Kuna watoto wa baadhi ya wakulima wenzetu wamekatisha masomo baada ya wazazi wao kushindwa kumudu gharama. Hawana fedha, chai ipo lakini soko la chai halipo.

"Yaani ni shida tupu tangu kiwanda kifungwe. Tunataka kiwanda kifunguliwe kwa sababu hapa watu wana mashamba mengi ya chai na wakulima ni wengi."

Katibu wa Chama cha Ushirika wa Chai Dule B, Zuberi Kaniki anakiri hali ni mbaya kiuchumi kwa wakulima kutokana na kukosa mahali pa kuuza chai yao.

Anasema kuwa zaidi ya vijana 200 waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho, wamekosa ajira baada ya kiwanda hicho kuuzwa kwa mwekezaji mwingine. Kaniki anasema vijana hao walilipwa stahiki zao zote na BBTCL baada ya kiwanda kuuzwa.

Rai yake kwa serikali ni kuingilia kati kuhakikisha kiwanda kinarejea katika uzalishaji ili wananchi wapate soko la chai yao, pia ujira kiwandani na uchumaji chai mashambani.



Sehemu ya mashamba ya wakulima katika Halmashauri ya Bumbuli, wilayani Lushoto. **PICHA: HALFANI CHUSI**



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

"Kama kuna kitu chochote kinakwamisha kiwanda hiki kuendelea kufanya kazi, iwe kwa makusudi au kwa kutokujua, tunaomba serikali itusaidie. Wakulima wa chai tunateseka sana!" Kaniki anasema.

Mwenyekiti wa Ushirika wa Chai Kata za Dule B na Mamba (UCHADUMA), Hiyob Shenkalwah (71), anasema wakulima hao wameathirika kutokana na kuuzwa kwa kiwanda hicho huku uzalishaji ukisitishwa.

"Chai nyingi katika mashamba yetu imeharibika, imekomaa kupitiliza. Kiwanda hiki (cha Herkulu Estate) kwa Bumbuli ni ajira, faraja, uchumi na furaha. Wakulima tunakitegemea kuendesha uchumi wetu," anasema Shenkalwah.

#### MHASIBU WA KIWANDA

Mhasibu Mkuu Jengo aliyekutwa na mwandishi kiwandani huko mwezi uliopita, anasema alipewa taarifa na bosi wake Septemba mwaka jana kwamba amewauzia Udongo Wetu Limited kiwanda hicho, hivyo abaki kiwandani huko kama mlinzi wa mali hadi pale mwekezaji huyo mpya atakapokwenda kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji.

"Ninachojua kiwanda kimeuzwa kwa mwekezaji mwingine, taratibu za kukabidhiana ndizo zinachelewa. Mimi na walinzi tumebaki hapa kuendelea kulinda mali za viwanda zisije zikaharibika kabla ya kumkabidhi mnunuzi," anasema.

Hata hivyo, Jengo anadai kutokuwa na taarifa sahihi kuhusu mchakato unaoendelea katika mamlaka za serikali kuidhinisha uuzwaji wa kiwanda, lakini akakiri kiwanda hicho kusitisha uzalishaji kumesababisha hasara kubwa kwa wakulima wa chai katika halmashauri hiyo.

"Mimi ninahuzunika sana kwa kuwa wakulima wa chai nimetoka nao mbali, nimekuja hapa nikiwa kijana kabisa, sasa nimeota mvi. Ninasikitika kwa hatua zilizochukuliwa juu ya kiwanda hiki. Wakulima wanapata tabu!

"Biashara ndogo hapa Bumbuli zimeyumba. Mimi mwenyewe nilikuwa nina laini tatu za uwakala wa fedha. Nimebakiwa na moja kutokana na mzunguko wa fedha kupungua.

"Tulitarajia kiwanda kingeanza tena uzalishaji mwaka huu, lakini hakijafunguliwa. Sasa tunajipa matumaini labda mwakani kitaanza tena uzalishaji," Jengo anasema.

Vilevile, mhasibu huyo anakosoa uamuzi wa baadhi ya wakulima kukata miche ya chai na kuanzisha kilimo cha miti ya mbao katika mashamba ya chai.

"Wawe na subira kwa sababu muda wowote kiwanda kinaweza kikafunguliwa. Si wakulima tu walioathirika, sisi (BBTCL) pia tumepata hasara, zaidi ya ekari 440 za kampuni zilizokuwa zimepandwa chai zimeharibika na jumla ya wafanyakazi 200 wa kiwandani na mashambani wamepoteza ajira," anasema.

#### MWEKEZAJI MPYA

Mhasibu Mkuu wa Udongo Wetu Limited, Nasri Hussein, anadai walishalipa fedha zote za kununua kiwanda hicho kwa BBTCL na wameshafuata hatua zote, ikiwamo kujaza fomu walizopatiwa na FCC, lakini hawajakabidhiwa kiwanda ili waendelee na uzalishaji.

"Sisi tumeshamaliza kila kitu, tumekwama FCC. Tunasubiri waturuhusu, tunasubiri baraka zao ili tukaendelee na uzalishaji. Tatizo nchini kwetu haya mambo ya uwekezaji huwa yanapelekwa taratibu sana," analalama.

Hussein anabainisha kuwa mbali na chai, wana mpango wa kuanzisha kilimo cha maparachichi katika eneo la kiwanda hicho, akisisitiza uzalishaji chai utaendelea kama kawaida.

"Tunatamani kikwazo kilichopo kitatuliwe mapema ili tuweze kuendelea na uzalishaji. Tulishapeleka malalamiko yetu Bodi ya Chai kwa ajili ya utatuzi wa suala hili," Hussein anasema.

#### BODI YA CHAI

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai, Beatrice Banzi, katika mazungumzo na mwandishi katika ofisi za bodi hiyo jijini Dar es Salaam Novemba 26 mwaka huu, alikiri kuwapo shida iliyosababisha kiwanda hicho kusitisha uzalishaji kwa zaidi ya mwaka sasa.

Alisema alishaongeza na uongozi wa kampuni ya Udongo Wetu, wakamthibitishia wameshamalizana na wenzao wa BBTCL, lakini kampuni hiyo ambayo wamiliki wake ni raia wa india, inadaiwa na FCC barua ya kuruhusu mchakato uendelee.

"Kilichobaki ni wao BBTCL kupeleka FCC barua ya makubaliano ili (tume) iamue na Udongo Wetu wakaendelee na kiwanda chao.

"Mpango uliopo sasa ni kuwakutanisha wote kwa pamoja FCC ili kutatua kikwazo kilichopo na Udongo Wetu aendelee na kiwanda chake," alisema.

Beatrice alifafanua kuwa kabla ya kuwaita wamiliki wa kampuni ya Udongo Wetu ofisini kwake ikiwa ni juhudi zake za kutaka kutatua changamoto hiyo, alishakwenda hadi ofisi za FCC jijini na kuzungumza na Mkurugenzi Mkuu, Willium Erio pamoja na Mkurugenzi wa Utafiti, Miungano ya Kampuni na Uraghibishi, Zaytun Kikula kuhusu kinachokwamisha kiwanda hicho cha chai kurejea kwenye uzalishaji.

Katika kushughulikia sakata hilo, Beatrice alisema aliwahi pia kumwandikia barua ya wito mmiliki wa BBTCL, lakini hakutii. Tayari alishaandika barua nyingine kumtaka afike ofisini kwao kisha waende naye FCC kuangalia mustakabali wa suala hilo.

Hata hivyo, mwandishi anafahamu kwamba Ijumaa iliyopita (Desemba 6, 2024), viongozi wa BBTCL, Udongo Wetu Limited na FCC walikwenda ofisi za Bodi ya Chai kuzungumzia suala hilo.

Baada ya kikao hicho, mwandishi wa habari hii alimtafuta Mkurugenzi Mkuu wa FCC, Willium Erio kuzungumzia suala hilo; naye akaelekeza ufafanuzi utolewe na Mkurugenzi wa Utafiti, Miungano ya Kampuni na Uraghibishi wa tume hiyo, Zaytun Kikula.

Baada ya maelekezo hayo, Zaytun alitoa ufafanuzi ufuatao: "Tulitoa tangazo la siku 14, ni kweli tuliletewa huo muamala, BBTCL na Udongo Wetu Limited wanajaua kwa sababu wao ndio walioleta hiyo 'transaction' na wanajua tuko katika hatua gani.

"Mchakato wa kupitia maombi yao unaendelea na kwa mujibu wa sheria huwa unachukua siku 90 hadi 135 baada ya hapo ndio tume inatoa uamuzi kupitia ripoti tutakayowakabidhi.

"Kwa hiyo, sasa inategemea na soko na washiriki wake, upatikanaji wake wa taarifa na kisheria ni siku 135 ambapo ndani ya siku hizo lazima tuhakikishe suala limefungwa na tume imeshatoa uamuzi.

"Lakini baada ya kuikabidhi tume ripoti ya uchambuzi, ina nafasi ya kufanya uamuzi wa aina tatu ambao ni kuruhusu, kuruhusu kwa mashatri au kuzuia muamala baada ya kupata ripoti ya uchambuzi na kuona muamala utakwenda kuleta faida au athari."

#### KAULI YA BBTCL

Jumamosi ya Novemba 30 mwaka huu, mwandishi aliwasiliana na Meneja wa BBTCL Tanzania, Pradhyuman Sight Bhat, kwa mtandao wa kijamii wa WhatsApp.

Alipotakiwa kutolea ufafanuzi kuhusu tuhuma zinazoelekezwa kwa kampuni yake kukwamisha uhamisho wa umiliki wa kiwanda cha chai huko Bumbuli, alisema:

"Mimi siwakilishi UWL (Udongo Wetu Limited) na siwezi kutoa maoni kuhusu maswali yoyote yanayohusiana na UWL. BBTCL ni kampuni iliyoorodheshwa nchini India na uongozi upo India, hivyo siwezi kusema lolote."

# YANGA KUMNG'OA KIUNGO WA SINGIDA BS USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI zimebaki siku sita tu kabla ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa, Klabu ya Yanga ipo kwenye hatua za mwisho kupata saini ya kiungo mkabaji matata wa Singida Black Stars, Kelvin Nashon.

Habari kutoka ndani ya Yanga, zinasema kuwa mchezaji huyo ana asilimia kubwa ya kujiunga na Yanga kwa mkataba wa mkopo wa miezi sita kutibu eneo hilo ambalo kwa sasa linaonekana kulegalega.

Mtoa taarifa huyo amesema Nashon, anakwenda kusaidiana na Khalid Aucho ambaye kwa sasa amekuwa akiandamwa na majeraha ya mara kwa mara, akicheza pia mechi nyingi ambazo zimeonekana kuathiri kiwango chake.

"Nadhani Nashon anaweza kutusaidia kwa sasa, tutamchukua kwa mkataba wa muda mfupi wa miezi sita, kama akifanya vizuri, basi mwishoni mwa msimu tutakaa na Singida Black Stars kwa ajili ya kufanya biashara nyingine, kwani tutamsajili kwa miaka miwili.

"Angalia hivi sasa kocha wetu, Sead Ramovic, ameamua kumchezesha Duke Abuya namba sita, wakati ni winga na kiungo mshambuliaji, kwa sababu tuna mapungufu kidogo kwenye eneo hilo, tunachohitaji ni ubora na Nashon timu zote alizoenda ameonekana yupo imara na kiwango chake hakishuki," alisema mtoa taarifa huyo.

Mbali na Aucho, raia huyo wa Kenya, Abuya, Yanga ina kiungo mkabaji mwingine, Aziz Andambwile, aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu akitokea Fountain Gate, lakini amekuwa hapati nafasi ya kucheza kwenye kikosi hicho.

Viungo wengine wawili, Mudathir Yahaya na Salum Aboubakar, wanaonekana kutumiwa zaidi kama namba nane, wakipanda kwenda kusaidia mashambulizi na kurudi kusaidia viungo wakabaji.

Habari zinasema huenda Yanga ikasajili wachezaji kadhaa na kuwaondoa wengi kipindi hiki cha dirisha dogo kutokana na mapungufu yaliyoonekana tangu mwanzo mwa msimu.

Viongozi wengi wa Yanga kwa sasa wapo nchini Algeria ambapo juzi timu yao ilicheza mechi ya raundi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kundi A dhidi ya MC Alger, na kuchapwa mabao 2-0.

## Fadlu ataja sifa majembe ya dirisha dogo

INATOKA UK. 24



mmoja kati ya wachezaji wataoibadilisha Simba kwa kiasi kikubwa kutokana na uwezo wake.

"Huyu jamaa ana uwezo wa kucheza winga zote mbili, ana uwezo wa kucheza nyuma ya mshambuliaji, anaweza kucheza kiungo mshambuliaji, ana kipaji halisi cha mpira mguuni, ukikaa kwenye miguu yake utaliona hilo, anaweza kuhadaa mabeki, ni hatari anapobaki na beki mmoja au wawili, na kikubwa kuliko yote, ana uwezo wa kupiga mashuti makali kutoka mbali. Ukiangalia mabao yetu mengi tumefunga ndani ya boksi, Mpanzu atakuja kuongeza kitu kikubwa na kama tukipata wengine kama yeye kwenye nafasi zingine tutaimarisha zaidi kwenye kikosi chetu ili kuwa hatari zaidi kwenye michezo ya kimataifa," alisema raia huyo wa Afrika Kusini.

Tetesi zinadai Simba huenda ikamsajili straika Mganda, Denis Omendi mwenye miaka 30 kutoka Klabu ya Kitara FC ya Uganda, ili kuongeza nguvu safu hiyo ambayo ina Mcameroon, Leonel Ateba na Steven Mukwala pia kutoka Uganda, kiungo mshambuliaji wa Orlando Pirates, Karim Kimviudi raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, pamoja na Abdelhay El Forsy kutoka Klabu ya Renaissance ya Morocco, ambaye anaweza kujiunga na Simba kwa mkopo wa mwaka mmoja.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

MAADHIMISHO

Ya Uhuru wa Tanzania Bara

Miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara:

*"Uongozi madhubuti na ushirikishwaji wa Wananchi ni msingi wa maendeleo yetu"*

63

TAREHE 09 DESEMBA 2024



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inaungana na Watanzania wote kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kuadhimisha Miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

218291402

Michezo
Jumatatu Desemba 9, 2024
Nipashe

## Amorim mambo magumu United

UKURASA 21



# YANGA: NAFASI ROBO FAINALI CAF BADO IPO

**Yaahidi kupigania pointi 12 zilizobaki huku ikipania kuanza kuzichukua kwa TP Mazembe kabla ya...**

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kipigo cha mabao 2-0 ilichokipata juzi kwenye Uwanja wa Julai 5, jijini Algiers nchini Algeria dhidi ya MC Alger katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Yanga imesema haijakata tamaa kwani kuna pointi 12 zilizobaki za kupigania ambazo zinaweza kuifanya timu hiyo kusonga mbele kwenye Kundi A na kutinga hatua ya robo fainali.

Akizungumza nchini Algeria, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amekiri kuwa hali ni mbaya na wapo kwenye wakati mgumu, lakini amesema ndiyo mchezo wa soka ulivyo kwani hata klabu kubwa kama Machester City ya England, inapitia kipindi kama hicho.

"Hayakuwa matokeo rafiki na hatukujiandaa nayo, huwezi kwenda kwenye michuano mikubwa kama hii ukiwa na matarajio ya kupoteza, lengo letu lilikuwa kushinda, lakini ndiyo maisha ya mchezo wa mpira wa miguu, ziko nyakati nzuri na zipo nyakati ngumu, sisi kama Yanga tunakiri sasa tupo katika nyakati ngumu.

"Tumeona hata Manchester City nayo haifanyi vizuri, inapitia kwenye wakati mgumu, kikubwa ni kurudi tena imara, haitakiwi hali hii kuendelea," alisema Kamwe.

Alisema kilichobaki ni kujipanga ili kuzipata pointi 12 zilizobaki katika michezo minne iliyosalia nayo ili kuweza kupata nafasi ya kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Naamini kwa ukongwe wa taasisi hii na uimara, tutarudi kwenye ubora wetu, matokeo haya yamemuumiza kila mtu, yamemuumiza mwalimu, benchi la ufundi, wachezaji na viongozi, lakini kwa kauli moja lazima tukubali ukweli, matokeo haya yanaweza kuikumba timu yoyote. Nyakati hizi zinapima watu uimara, wanachama na mashabiki wa Yanga wanatakiwa kuwa watulivu, tujiandae kwa mchezo unaofuata ili kurudi kwenye reli.

"Tunahitaji pointi 12 zilizobaki kusonga mbele, tunaamini tunaweza kuzipata kama tutajipanga," alisema Kamwe.

Yalikuwa ni mabao ya Ayoub Abdellaoiu dakika ya 64 na Sofiane Bayazid dakika za nyongeza kabla ya mechi kumalizika, yaliifanya timu hiyo kupoteza mechi mbili mfululizo kwenye Kundi A, baada ya kupoteza kwa idadi kama hiyo ya mabao, Novemba 26, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kuendelea kuburuza mkia kwenye kundi.

Yanga sasa imebakisha michezo mitatu dhidi ya TP Mazembe utakaochezwa, Desemba 14, mwaka huu, nchini DR Congo na kurudiana Januari 3, ambapo Januari 10, itakuwa ugenini dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, kabla ya kumalizia mchezo wao wa mwisho nyumbani dhidi ya MC Alger, Januari 17, mwakani.



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua (kulia), akiachia shuti kali huku beki wa MC Alger ya Algeria, akiwa makini kuzuia kwenye mechi ya Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Julai 5 jijini Algers juzi na wenyeji hao kushinda mabao 2-0. **PICHA: YANGA**

## Fadlu ataja sifa majembe ya dirisha dogo

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema anahitaji kujaza nafasi chache tu za wachezaji kipindi cha dirisha dogo, lakini ni kwa wachezaji ambao wataingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza na si wa kuja kukaa benchi.

Fadlu, amekiri kuwa winga wa timu hiyo, Elie Mpanzu ni mchezaji ambaye wataingia moja kwa moja kwenye kikosi kutokana na jinsi alivyomuona tangu siku ya kwanza na kila anavyozidi kufanya mazoezi, anazidi kumshawishi kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza.

"Ni kweli nahitaji wachezaji wachache kwenye kikosi changu kipindi cha dirisha dogo la usajili, lakini ni wale ambao wakija wataingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza. Kama watakaa nje basi itakuwa hivyo kwa sababu ya mifumo, kupumzika, au sababu nyingine ya kikosi kipana, lakini si kwa sababu ya kiwango kidogo.

Kuna timu ambazo zina kikundi cha wachezaji wachache wana uwezo ambao wanafanya kazi ya wenzao, wengine viwango vyao ni vidogo, wanabebwa na wenzao, unaweza kuona mapungufu hayo pale wale wa kikosi cha kwanza watakapoumia," alisema Fadlu ambaye amesifika kwa kuinua viwango vya baadhi ya wachezaji ambao hapo awali walikuwa hawachezi, pia kutumia idadi kubwa ya wachezaji waliosajiliwa msimu huu mpaka sasa.

Alisema ni bora abaki na wachezaji waliopo sasa, kuliko kuletwa wachezaji ambao watakuja moja kwa moja kukaa benchi na kusubiri wenzao waumie ili wacheze.

"Unaona kwa sasa kwenye kikosi changu kuna mtifuano wa kuwania namba, kwa sababu kila mmoja ana kiwango kizuri, wengi wao nimewakuta, lakini wale ambao watasajiliwa chini yangu ni lazima nijiridhishe kuwa kiwango chao ni cha kuichezea timu ya Simba na ana uwezo wa kuingia moja kwa moja kikosi cha kwanza," alisema.

Akitoa mfano wa Mpanzu, alisema hakuna shaka yoyote kuwa ni

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >